Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 12 Julai, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika,(Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nawaomba tuzingatie sana muda, hali yetu sio nzuri juu ya ratiba yetu na namna ambavyo tunaendelea na shughuli zetu. Nawaomba sasa nimkaribishe Mhe. Ussi Jecha Simai na baadae, inabidi niwe natafuta tafuta maana watu wenyewe siwaoni. Hebu tuendelee kwanza. Mhe.Ussi Jecha Simai.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya mwanzo hii leo ya kuchangia hotuba ya bajeti iliopo mbele yetu. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti hii pamoja na watendaji wote wa wizara.

Moja kwa moja Mhe. Spika, mimi naanza kutoa mchango wangu katika kitabu hiki kwenye idara ya nyumba na maendeleo ya makaazi, ukurasa wa 29 hadi 32. Mhe. Spika, katika mijadala mbali mbali niliyokuwa nikichangia sana kuhusu nyumba za maendeleo ambazo zimejengwa na Marehemu Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Karume. Miongoni mwa nyumba hizi Mhe. Spika, tunazo pale Gamba pamoja na maeneo mengine mengi tu ya Shamba. Mhe. Spika, nyumba hizi zimejengwa kwa gharama kubwa sana, lakini hivi sasa nyumba hizi nyingi zao zimekuwa zikivuja.

Mhe. Spika, katika michango yangu mingi niliyokuwa nikichangia nilimtaka Mhe. Waziri ajaribu kuangalia suala la kuziezeka nyumba hizi, kwani nyingi zao zinavuja kwa sasa. Pia nyumba hizi hasa zile za Gamba makaro yake kwa sasa ni mabovu na yanapelekea mpaka kuhatarisha afya za wananchi wetu katika maeneo haya.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze, serikali ina mpango gani katika kuzirekebisha nyumba hizi ili wananchi wetu waweze kuishi vizuri kwa usalama na amani.

Mhe. Spika, pili moja kwa moja nitakuja kwenye Mamlaka ya Maji, katika ukurasa wa 37 hadi 49. Mhe. Spika, kila siku tukifika hapa basi mimi ninakuwa na kilio cha maji katika Jimbo langu la Chaani. Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Chaani kuna ahadi nyingi zimetolewa. Kwanza kuna ahadi ya Rais Mstaafu Dk. Amani Karume, ambayo aliitoa Moga Mwembe Mkali kwamba atawachimbia kisima cha maji, tangu mwaka 2008, lakini mpaka leo hii Mhe. Spika, kwa bahati mbaya jambo hilo bado halijatekelezwa.

Vile vile kuna ahadi ya Rais Mhe. Dk. Shein ambayo aliitoa mwaka 2010, kwamba atawachimbia kisima watu wa Moga Mwembe Mkali hadi hivi sasa bado. Lakini kuna ahadi nyingine Mhe. Spika, ilitolewa Banda Maji mwaka 2008 na aliyekuwa Waziri wa maji wakati huo.

Mhe. Spika, pia kuna ahadi mwaka 2010 ilitolewa pale Kinyasini kwamba watachimbiwa kisima, lakini hadi hivi sasa bado. Katika kitabu hiki Mhe. Spika, nimeona visima hivi vimetajwa, lakini kutajwa kwa visima hivi ni kawaida ya wizara ya maji kuvitaja kila siku. Mwaka jana, mwaka juzi na hii ni bajeti ya tatu vinatajwa visima vya maji Kinyasini au Bandamaji lakini utekelezaji kwa kweli hamna.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi leo sitokuwa rahisi sana kukubali kupitisha kifungu cha Mamlaka ya Maji, ikiwa Mhe. Waziri hatoniambia lini, kwa sababu aniambie ni lini, kabla ya mwezi wa Oktoba basi mimi nione jitihada zake kwamba zinafanywa na ndio niamini kama kweli Mhe. Waziri ana nia ya kutaka kuwapatia maji watu wangu wa Jimbo la Chaani, hasa pale Moga na Kinyasini au Bandamaji.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende kwenye Shirika la Umeme. Katika kikao kilichopita, Mhe. Waziri aliahidi kwamba tushirikiane katika bajeti hii atawapatia umeme watu wangu wa Moga Kirama. Nilimueleza kwamba mwaka juzi tulinunua nguzo, lakini kwa bahati mbaya Shirika la Umeme walikuja kutuambia kwamba nguzo hizi hazifai. Juzi katika swali langu la nyongeza akaniambaia kwamba katika bajeti hii, bajeti hii tayari ndio tunaipitisha hivi sasa. Kwa kuwa sisi tuko tayari kusaidiana na shirika, kama nilivyomuahidi Mhe. Waziri, nilimuambia kwamba mimi niko tayari ama sisi viongozi wa Jimbo letu tuko tayari pamoja na wananchi wetu kuchangia au kushirikiana na Shirika la Umeme ili watupatie huu umeme.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, leo nataka akija hapa Mhe. Waziri aniambie ni lini, kwa sababu sisi sasa hivi tuko tayari kuchangia ama kusaidiana naye katika suala hili, hata akituambia kesho yeye atakuwa tayari tushirikiane au tusaidiane, sisi tuko tayari. Kwa hivyo, atakapokuja hapa akinieleza tu kwamba kesho asubuhi tutoke, tutoe pesa zetu za kuchangia basi sisi tuko tayari. Laa kama sitopata majibu mazuri katika eneo hili basi mimi sitokuwa tayari kupitisha fungu hili.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda wako unauengaenga sana, kwa sasa basi mimi niishie hapa, nakushukuru sana. Kwa hivyo, sitounga mkono hoja hadi pale Mhe. Waziri atakaponipa majibu mazuri ya kuridhisha ndani ya miezi mitatu hii hapa, ahsante sana Mhe Spika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka huu wa 2013/2014.

Mhe. Spika, tunaelewa kwamba sekta ya ardhi ina majukumu ya kusimamia rasilimali ya ardhi na kuangalia matumizi bora ya ardhi, na hii ni kwamba sisi tunaitegemea ardhi iweze kutusaidia, na kwa sababu ina mchango mkubwa sana ardhi, wakati ambapo tunaweza kuitumia ardhi kwa kuwakodisha wawekezaji. Vile vile tunapata fedha za kutosha na kwa wawekezaji tunapata fedha za kutosha, pia itaweza kusaidia uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, ardhi tuliyonayo ni lazima tuigawe kwa kuzingatia mahitaji yote ya jamii, pamoja na huduma na kutekeleza miundombinu iliyokamilika. Hili ni jambo ambalo Mhe. Waziri ni lazima atimize ahadi hii kabla ya ujenzi mpya kufanyika, ni lazima ahakikishe kuwa huduma zote zinazohitajika zinatekelezwa.

Mhe. Spika, idara ya ardhi imepima viwanja vingi visivyopungua 543 kwa Unguja na Pemba. Katika viwanja hivi wameweza kuvizingatia mahitaji yote muhimu kwa vijiji mbali mbali, na katika ugavi huu wa viwanja vyote hivyo 523, viwanja vya makaazi ni viwanja 343, viwanja vya huduma ni 27, vimeingizwa vitega uchumi pia navyo viwanja 24, taasisi za serikali viwanja 49 na sehemu ya kilimo 80. Kwa hivyo, vyote hivyo vinafanya jumla ya viwanja ambavyo vilikuwa vinahitajika ni 523.

Mhe. Spika, miongoni mwa viwanja hivi ni pamoja na maombi ya watu binafsi na vile vile taasisi mbali mbali. Namshukuru Mhe. Waziri kwa kuweza kufikiria kwamba maombi ya wananchi yalikuwemo na vile vile tuzingatie na taasisi za serikali.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wizara itakuwa imejiandaa katika masuala ya miundombinu yote imekamilika, kwa kuzingatia hali halisi ya kuweza kupata maji, barabara na umeme. Ni jambo la kufurahisha na kumshukuru Mhe. Waziri kwa kujiandaa kwa masuala kama hayo muhimu ya barabara, maji pamoja na umeme. Sasa hivi kwa kuanzia nafikiri itakuwa ni Tunguu mahala pa mwanzo ambapo suala hili litaweza kutendeka.

Mhe. Spika, tuizungumze hali halisi ya mradi ambao umepita nyuma kwa miaka kadhaa iliyopita. Wizara ilijiandaa na *master plan* na wizara kwa kipindi hicho ilipokuwa *master plan* imetayarishwa, inaonesha kwamba wizara kabla ya kukamata yeye Mhe. Waziri aliyepo hivi sasa, lakini haya ni mambo ya zamani ya miaka ya nyuma ya miaka ya 1980, lakini ilionekana *master plan* kwa Zanzibar ilikuwa ipo. Ilionesha kwamba wizara ilishindwa kuitekeleza hii Zanzibar ki- *master plan*. Sasa naomba kwa yeye Waziri aliyepo hivi sasa kama ataweza kunipatia jibu ni sababu zipi za msingi zinazosababisha kurejesha nyuma suala hili, kwamba *master plan* ilikuwa tayari na zaidi ya miaka 10 au 15 haikuweza kutekelezwa, nilitaka nijue kwa nini ikawa hivyo.

Mhe. Spika, vile vile nilitaka kujua kwa kuwa serikali ilishindwa kudhibiti ardhi, pamoja na usimamizi mbovu, tamaa ya watendaji na watu binafsi, kwa hivyo ardhi ilipata hujuma kubwa sana, kuuzwa ardhi hii kwa bei kubwa, ikaanza kutolewa viwanja bila ya kuwa na *plan* yoyote, yaani vilikuwa vinatolewa kiholela tu. Je, Mhe. Waziri kwa kipindi hicho katika matokeo ya ujenzi holela usiokuwa na mpango wa kisheria, ni hatua gani zilichukuliwa baada ya kuchunguzwa kuwa miji iliyojengwa haikuwa ya mpango mzuri, ambayo tunaita hii ni *unplanned settlement.* Je, ni hatua gani Mhe. Waziri alichukua.

Mhe. Spika, katika ujenzi naamini vibali vinatolewa. Suala la vibali kutolewa na mji ulikuwa unaonesha unajengwa na wizara au idara inayohusika na ujenzi ilikuwa ipo, kwa nini vibali hivi vilikuwa vinatolewa na huyu mtoa vibali hakujua kuwa ni lazima kutakuwa na utaratibu maalum wa kujenga, akaruhusu watu kujenga nyumba ovyo bila kuzingatia mahitaji maalum.

Je, huyu mtoa vibali alichukuliwa hatua gani na baada ya hatua hizo hakuna taarifa zozote zilizokuwa zimeandaliwa. Bila shaka vibali vilipokuwa vinatolewa baada ya kuonekana hivyo, basi vibali vilisitishwa. Nataka kumuuliza Mhe. Waziri ni mwaka gani vibali vilianza kusitishwa.

Mhe. Spika, nataka vile vile nipate maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri, fedha ambazo alikuwa ametenga katika kuboresha miji hii yote pamoja na vijiji ni kiasi gani cha fedha ambacho kitahitaji kukidhi mahitaji ya ujenzi mpya.

Mhe. Spika, pia nataka kujua kutoka kwa Mhe. Waziri je kuna misaada yoyote kutoka kwa washirika wa maendeleo, kama kuna misaada tunataka kujua ama serikali tu ya Zanzibar inajitegemea peke yake pia tulitaka tujue.

Mhe. Spika, tumepata taarifa hapa kwamba katika masuala yote kumetokezea migogoro ya ardhi, ambapo migogoro hii ilikuwa ni mingi sana na kesi zilikuwa ni nyingi. Kati ya kesi ambazo zilikuwa na migogoro ni 94, ni kesi 45 tu ndizo zilizoweza kuchukuliwa hatua mpaka sasa hivi.

Je, Mhe. Waziri huoni kama dhulma imepita juu ya migogoro ya ardhi, kama kesi ni 94 na zimepelekwa mahakamani, hii inaonesha kuwa watu wamedhulumiwa, hii ni dhulma maana yake mtu pengine ni ardhi yake, vibali vinatolewa kiholela, ujenzi unajengwa kiholela, mtu kanyang'anywa ardhi yake, basi imebidi watu kupelekana mahakamani.

Je, Mhe. Waziri, huoni kama hawa wametenda kosa kwa kuchukua haki ya mtu, sio jambo zuri. Mahakama bila shaka zilikuwa zinaendesha kesi na bado watu wanalalamika mpaka leo kuwa wizara imechukua jitihada gani ya kusimamia masuala haya. Bado watu ambao wamedhulumiwa, maeneo yaliyochukuliwa na kesi pengine anaambiwa mtu yule wewe sio yako, lakini bado mtu yule aliyechukuliwa ardhi yake bado anaendelea kulalamika. Je, wizara hii inayasimamia haya masuala kwa kiasi gani.

Mhe. Spika, katika kupanga miji mipya pamoja na vijiji, tujaribu kuepukana na migogoro ya ardhi. Nilitaka kujua tu katika mambo haya ya miji mipya, wizara yako imewashirikisha kwa kiasi gani. Kwa mfano Mamlaka ya Mji Mkongwe, Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya, kwa sababu haya maeneo manne ni muhimu sana, na kwa sababu hawa kama hawatoshirikishwa vya kutosha, basi kunawezekana kwamba migogoro ya ardhi ikaweza kuendelea tena, pamoja na kutengeneza miji mipya.

Mhe. Spika, kwa wale ambao wanapenda kupata kumbukumbu za kihistoria juu ya maendeleo ya ujenzi mpya, mipango miji. Je, taarifa za mji mpya ni pahala gani zinaweza kupatikana. Je, taarifa hizi mpya zinaweza kupatikana kutoka kwako wewe Waziri katika wizara yako au taarifa hizi zinaweza kupatikana *archives*.

Kwa mfano, kuna taarifa zile za ardhi, taarifa za usajili, kumbukumbu za mazingira na uhakiki wa ardhi. Mambo kama haya manne yanaweza kupatikana wapi, kama mtu anataka kuipata historia ya Zanzibar katika ujenzi wa kale ambao uliokuwa.

Mhe. Spika, tunaamini kwamba ifikapo mwaka 2015 sekta ya ardhi itakuwa tayari imeshatumia kiasi cha asilimia 50 ya ardhi ya Zanzibar kwa ajili ya uzalishaji na uchumi wa Zanzibar. Sasa kwa mwenendo huu na baada ya kufika miaka 13, 15 au 20 ijayo, ardhi kama sehemu ya maisha yetu ambayo inaweza kutuongezea au kuongeza vizazi, vizazi vinazidi kuongezeka kila siku kwa haraka sana.

Je, ardhi ya kulima haitokuwa mtihani kwa raia wa Zanzibar? Kwamba kila siku ardhi hii tunaanza kuikata kwa ajili ya majenzi na kama unavyojua ardhi katika kisiwa chetu ni ndogo. Je, hatuoni huo utakuwa ni mtihani wa baadae baada ya miaka 20, tunayo tathmini ya kutosha kuweza kuelewa baada ya miaka 20 tunaendelea na majenzi kila siku na sehemu ya ardhi ya kulima inaanza kutoweka. Je, Mhe. Waziri kuna tathmini yoyote ambayo umefikiria kwa mipango ya baadae kwa ajili ya wananchi?

Mhe. Spika, baada ya hayo nataka kuzungumzia suala zima la ufungaji wa mita

Mhe. Spika: Kwa dakika tano.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: *Inshaallah*. Katika ufungaji wa mita, sisi tuliahidiwa hapa kwamba mita tutatiliwa na mpaka leo bado mita hatujatiliwa.

Vile vile nilitaka kumuambia Mhe. Waziri kwamba mimi katika Jimbo langu, hii ni mara ya pili, au mara ya tatu au mara ya nne naomba tangi la maji ambapo niliwahi kutoa taarifa kwamba tangi hili la maji ni bovu na haliwezi kukidhi haja kutokana na idadi ya nyumba pamoja na idadi ya watu walivyokuwa wengi. Majenzi ambayo katika tangi hili, yalikuwa ujenzi wake hauwezi kutoa presha kubwa ya maji, tangi liko chini kwenye ardhi. Je, Mhe. Waziri naomba unipatie taarifa ni lini hasa Konde wataweza kupatiwa tangi la maji.

Mhe. Spika, vile vile nataka kumwambia Mhe. Waziri katika mazungumzo ya miaka kadhaa ya Baraza hili, niliweza kuzungumzia kwamba kuna vijiji vyangu visivyopungua vitatu au vinne vinahitaji umeme na mpaka leo bado utekelezaji wa umeme katika vijiji hivyo haujapatikana.

Kwa mfano vijiji vya Gombani, vijiji vya Ungi, Kivumoni pamoja na Chaleni. Vijiji hivi vimeshindikana kupatiwa umeme. Kwa hivyo, napenda nimuulize Mhe. Waziri ni lini nitapata huduma hii ya umeme kwa wananchi.

Mhe. Spika, pia nataka kujua kuhusu suala zima la Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kuna nyumba ambazo ziko katika Idara ya Ujenzi, mpaka

leo nyumba hizi ambazo kwa amri ya Rais katika miaka iliyopita ilikuwa watu ambao waliweka amana kwenye wakfu, nyumba hizi zilikuwa ziwe chini ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na mpaka leo nyumba hizi bado idara yake hawajazipeleka kwenye Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri je, ni lini Idara ya Nyumba itakabidhi rasmi nyumba hizi kwa Kamisheni ya Wakfu ambapo ni jambo la msingi?

Mhe. Spika, kwa muda wa dakika tano, nategemea dakika tano zimemaliza na mimi nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu, ahsante na mimi naunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri ahsante sana.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii adhimu ya kuzungumza machache na kuchangia katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia leo kufika hapa tukiwa na afya njema. Pili nimpongeze Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa matumaini makubwa na vile vile imejaa mipango ambayo tunaamini kwamba kwa uwezo wake Allah yanaweza kutekelezeka. Kwa hivyo, nampongeza sana pamoja na watendaji wake wote wa wizara, ambao kwa kweli wameshirikiana katika kutayarisha bajeti hii.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi sana ya kusema kwa sababu wenzangu waliotangulia wameshayagusia mengi na ningependa zaidi kuyagusia yale ambayo ninahisi kwamba nitatilia mkazo, lakini vile vile nahisi kwamba bado hayajachangiwa.

Mhe. Spika, mimi naanza na ukurasa wa 13 ambao ni wa Ofisi ya Mrajis wa Ardhi. Mhe. Spika, kwanza ninapongeza sana wizara kwa hatua mbali mbali ambazo zimechukuliwa kwa kuweza sasa kufanya usajili wa ardhi mbali mbali zikiwemo za nyumba na ardhi.

Lakini Mhe. Spika, naomba nimuambie Mhe. Waziri kitu kimoja, kwa sababu nimepata wasi wasi mkubwa kuhusu suala la usajili huu hasa kwa watendaji ambao wanashughulikia usajili. Mhe. Spika, jana hapa Mhe. Saleh Nassor alizungumza suala la mtu mmoja ambaye ana asili ya Kiarabu kubaguliwa, kwa kuwa aliambiwa hatopewa ardhi kwa sababu ni Muarabu.

Mhe. Spika, mimi imenisikitisha sana na ningemuomba sana Waziri kama yupo mtu kama huyo basi achukuliwe hatua haraka iwezekanavyo. Mhe. Spika, hii ni cheche ndogo sana ya moto, lakini cheche hii inaweza kuzua moto mkubwa. Kwa kawaida Zanzibar kumekuwa na kabila nyingi na tumeishi kwa muda mrefu na hakuna ubaguzi. Kwa sababu mimi nakumbuka vizuri sana kwamba kuna maeneo mengi ambayo yanamilikiwa na Waarabu na wana kila haki na katiba yetu ya Tanzania pamoja na ya Zanzibar, inasema kwamba "watu wote ni sawa na wote wana haki sawa".

Mhe. Spika, sasa ikiwa mtendaji mmoja anajitokeza kusema kauli kama hii, kwa kweli Mhe. Waziri mchukulie hatua kali, kwa sababu vile vile inaweza kuleta taswira mbaya kwa nchi yetu, hasa tukianza mambo ya kubaguana. Dunia ya sasa tuko katika utandawazi tunaonekana, tunachokisema hapa watu wanakichukua na kinaweza kuenea na kuleta hasara kwa taifa letu. Hili ni jambo hatari sana, nasema ni cheche ndogo lakini inaweza kusababisha moto mkubwa kiuchumi na kisiasa.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri, jambo lile mimi halikunipa usingizi hata kidogo. Nataka liwekwe wazi ili ujulikane ukweli kwamba mtu amebaguliwa na lisije kuachiwa, kwa sababu likiachiwa hili na mara nyingi tunafanya makosa hayo, kwa sababu wanaachiwa watu kufanya maovu, hawahukumiwi na baada ya hayo na kuna wengine wanatokea wanafanya hilo hilo. Ubaguzi kama huu sisi hatuutaki, tumeukataa zamani na mara nyingi sana tunasema kwamba kila mtu apewe haki sawa, kwa sababu kila Mzanzibari ana haki ya kumiliki ardhi. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nitakwenda katika ukurasa wa 49, nilisema sizungumzi sana, isipokuwa nitazungumza mambo mawili kwa sababu mengi yameshazungumzwa na mengine watakuja wenzangu kuyazungumza.

Mhe. Spika, ni suala zima la Idara ya Nishati na Madini. Kwa kweli idara hii ni changa kwetu sisi hapa Zanzibar na changa kwa sababu bado hatujaanza hasa kuifanyia kazi. Lakini kilio kikubwa Mhe. Spika ni elimu, bado hatujaweza kujipanga kuhakikisha kwamba tutapata wataalamu kutoka hapa kwetu Zanzibar.

Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ahakikishe hivi sasa tunaanza kujitayarisha katika kufundisha vijana wetu, ili waweze kuchukua nafasi kwenye sehemu hizi na hususan katika maeneo ya nishati na madini. Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu ni vyema tuanze kujipanga na sio tu tuanze kujipanga kwa kuanza kutayarisha vijana ambao tayari wamemaliza, isipokuwa tuanze kutayarisha vijana, ambao elimu

ya msingi tuanze kuwapatia mafunzo mazuri pamoja na elimu nzuri kuhusiana na masuala haya.

Vile vile nimeona hapa kuna watu ambao wamepelekwa nje kusoma *UAE* na hapa Tanzania vipo vyuo mbali mbali hapa Tanzania. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba tunao wanafunzi ambao wanahitimu au wanamaliza vizuri masomo ya *science*. Sasa wanafunzi hawa kwa kuwa tunawahitaji sana basi tuhakikishe kwamba wanapewa *priority* kwenda kusoma masomo ambayo baadaye yatakuja kuleta mafanikio na maendeleo katika nchi yetu.

Baada ya hayo, mimi napenda kumpongeza sana Mhe. Waziri, kwa sababu nimeona mipango yake mizuri. Lakini naomba kuongeza jambo jengine moja ambalo linahusiana na ukataji wa maeneo mbali mbali ikiwemo maeneo ya makaazi, kilimo, huduma. Mhe. Spika, hapa nataka kujua kwamba anakusudia nini Mhe. Waziri anaposema huduma, kwa sababu katika kueleza amesema wanayo maeneo kama mia tano na kidogo yanayozungumzia suala zima la makaazi, taasisi za serikali pamoja na maeneo ya huduma, lakini maeneo ya huduma nimeona ni kidogo sana.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anielezee, kwa nini hizi sehemu za kutoa huduma ni kidogo sana, pia ana maana gani akisema ni huduma, kwa sababu huduma tunavyofahamu sisi ni huduma zote za kijamii. Kwa mfano, misikiti, maduka, skuli, hospitali, viwanja vya kuchezea watoto ambavyo ndio muhimu sana ambapo mara nyingi sana, kwani ni muhimu kwa vijana wetu ambao wanahitaji maeneo ya kufanyia michezo, ili waepukane na maovu ambayo yanafanyika hivi sasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja basi atuelezee na halafu aniambie kwa nini hizi nafasi zimekuwa kidogo mno za kutoa huduma? Na hapa sijaona na ingekuwa ni suala jengine kama vile maeneo ya michezo au mengine. Lakini hapa kwa kweli sijaona maeneo ya michezo au skuli, kwa hiyo na hilo pia naomba kupata maelezo yake Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nafikiri mpaka kufikia hapa na majibu mengi yanapatikana kwenye kitabu ninampongeza sana Mhe. Waziri, kwa sababu nimeona kwamba mengi nilikuwa nikijiuliza hapo mwanzo, lakini baadaye nimekuta kwamba majibu mengi ambayo yanapatikana kwenye kitabu hichi.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 90 na naziweka asilimia zangu 10 mpaka hapo nitakapopata majibu ya kuniridhisha. Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunakushukuru. Kwa hivyo, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Fatma Mbarouk Said, baadaye Mhe. Abdalla Juma Abdalla wakati Mhe. Hassan Hamad Omar anajitayarisha.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa hii adhimu kwa siku ya leo mwezi tatu Ramadhani kwa kweli nakushukuru sana. Pia namuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kuzifunga hizi kwa salama na amani na zitakabaliwe *Inshallah*.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia hotuba yake hii ya bajeti ya mwaka 2013/2014 pamoja na watendaji wake. Mhe. Spika, naomba niseme kwamba kwa Mhe. Waziri huyu, basi naamini kwamba haya ambayo ametuletea hapa kwa kweli ni mtu ambaye nimekaa naye kwa muda mrefu, kama nilivyokuwa ni mfanyakazi wa serikali basi aliwahi kuwa Waziri wangu kwa mara mbili; nikiwa Wizara ya Habari, pia nikiwa Wizara ya Katiba na Utawala Bora na baadaye nikahama pale nikaenda Wizara ya Elimu.

Kwa hivyo, naamini kwamba utendaji wake ni mtu muadilifu sana, yaani watu wawili hawa mimi kila pahala nitakapokwenda naangalia utendaji wake wa kazi, na si hayo ni mtu ambaye niko karibu naye. Kwa mfano, hata nikienda nyumbani kwake nyumba zake zote mbili nikienda hivi sasa nitakaribishwa kwa nidhamu kabisa, kwa kweli ni mtu ambaye niko karibu naye. *(Makofi)*
Mhe. Spika, watu wawili hawa akiwemo yeye na niseme hapa Rais wangu Dkt. Ali Mohammed Shein ni watu ambao ni waadilifu sana, kwa sababu nilipokuwa nikifanya kazi nao kwa kweli hawakunipa tabu, na kwa sababu nilikuwa Mshika Fedha Mkuu, hivyo sikupata tatizo lolote kutoka kwao wao na kama vile akichukua *imprest* basi anarejesha. Kutokana na hali hiyo, inaonesha kwamba ni mtu mkweli na muwazi. *(Makofi)*

Baada ya hayo, niende kwenye ukurasa wa tatu niliona hapa, ingawaje Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ameelezea, kwamba mapato yale iliyopangiwa kukusanya wizara hii ni bilioni 4,092,000,000/= lakini mpaka tarehe 31 Machi, 2013 zimekusanywa jumla ya bilioni 1,979,365,755/=. Kwa kweli *gape* hapa ni kubwa na karibu bilioni 2,113,634,245/= na hata ukijumuisha miezi mitatu ambayo ni Aprili na Juni bado itakuwa hazikufikia lile lengo, ingawaje Mhe. Mwenyekiti amesema kwamba kulikuwa na mapungufu haya yaliyotokana na viwanda vya kokoto havikuwa vizuri.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri ananieleza tu hali hiyo ambayo Viwanda vya Kokoto haikuwa nzuri kutokana na nini fedha au ni jambo gani? Basi aje anieleze Mhe. Waziri.

Suala jengine ni kwamba niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, kuwa wizara hii ina mambo mengi na mazito.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naona kama sauti zinachanganyika hivi. Mhe. Mjumbe, endelea kuchangia.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, wizara hii ina majukumu mazito, maji, nishati ikiwemo umeme.

Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwa juhudi kubwa ambayo inajitahidi kwa kuwaletea maendeleo wananchi wake na kuwaondolea matatizo ya hapa na pale. Kwa hivyo, mambo haya ni muhimu ya maji na umeme, kwani bila ya kuwa na maji hatuwezi kuishi. Sasa sisi kama viongozi na tumechukua jukumu la kujinadi kwa wenzetu kwamba suala la maji ni muhimu.

Kwa hiyo, ninaomba pale tunapochukua fursa au tunapoomba suala la kuongeza, basi ni jukumu letu kuona kwamba wananchi wetu wanaondokana na matatizo yale, pia kwa kuisaidia serikali huwa tunaomba kuchimbiwa visima katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri azungumze na watendaji wake, awashajihishe na wao, ili pale tunapotaka kuisaidia serikali, kwa sababu tumeona miradi ni mingi. Lakini mpaka leo bado maji ni tatizo kwa visiwa vyetu hivi pengine ni kutokana na ongezeko la watu, ama upungufu wa maji au miundombinu kama ni mibovu, na sisi pia tunalo jukumu la kuondosha tatizo hili kama ni wananchi wa nchi hii, ili kuwaondoshea matatizo haya.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la uchakavu wa majengo, ambayo yanamilikiwa na serikali kama vile Nyumba za Michenzani. Mhe. Spika, hali si nzuri sana na hasa haya majengo ambayo yaliyojengwa miaka ya 1960, na kwa sababu ya uimara basi yalikuwa na viwango, lakini yanavyoonekana hivi sasa ni kwamba yamechakaa sana.

Kwa hivyo, serikali ichukue juhudi sana kuyafanyia ukarabati majengo haya. Kwa mfano, hata hivi sasa kwenye ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu mara nyingi anakagua pia na ule uhifadhi wa vitu vyenyewe. Kwa hiyo, haitakuwa vizuri sana kuyaacha majengo haya yakachoka sana, na kwa sababu usipoziba ufa utajenga ukuta. Kutokana na hali hiyo, kila mara yawe

yanapitiwa, kwa ajili ya kuyafanyia marekebisho na kuepuka kutumia fedha nyingi wakati tunapofanya marekebisho. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa sababu wenzangu mengi wameshayazungumzia, lakini nataka nizungumzie kuhusu suala la hati miliki. Kwa kweli suala hili limekuwa ni tatizo na wala hatujui ni wapi au mhusika ni nani. Kwa mfano, kuna majengo na hasa ya serikali yanakosa hati miliki na ukienda huko basi hujui umkamate nani.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, afanye juhudi ya kuyapatia hati miliki haya majengo ya serikali.

Vile vile Mhe. Spika, nikienda kwenye migogoro ya ardhi. Kwanza kwa maelezo ya Mwenyekiti wa Kamati ambapo ametusaidia sana kwamba kuna mapungufu ya Mahakama ya Ardhi. Kwa kweli ardhi imekuwa ni tatizo sugu, licha ya ile migogoro baina ya mtu na mtu.

Lakini mimi ninachokiomba zaidi kwamba ile migogoro inayohusu serikali labda na taasisi. Mimi nadhani Mhe. Waziri akae na kuona kwamba migogoro hii haiwezi kutokea na hasa kwa upande wa serikali iwe inajidhatiti sana.

Mhe. Spika, pia wizara itoe elimu kwa wananchi, kwa sababu migogoro mingi ya ardhi inatokana na kutojua sheria, yaani Sheria za Ardhi watu hawazijui na mtu atang'ang'ania pahala kwamba ardhi hii hivi na vile na watu kuleta migogoro, lakini baadaye ukichunguza utaona hawajui hata ile Sheria ya Ardhi. Kwanza kisheria Ardhi ni mali ya serikali, lakini mtu atakwambia hapa ni sehemu yangu, lakini ukimuuliza hata ile hati ya kumiliki ile ardhi hana.

Baada ya hayo, Mhe. Spika na kwa sababu naheshimu sana muda wako, basi naomba kuunga mkono hoja ya hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mhe. Abdalla Juma Abdalla, baadaye Mhe. Hassan Hamad Omar, wakati Mhe. Mlinde Mbarouk Juma anajitayarisha.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niseme mawili matatu. Kwanza mimi naanza *Bismillah* kwa kusema siungi mkono hoja, na siungi mkono kwa sababu moja tu Mhe. Spika, kwamba hii ni bajeti ya nne au ya tano na kila ninapozungumza huwa ninazungumzia kijiji changu cha watu wa Ngomeni, kwa kweli watu wa

Ngomeni serikali imewatelekeza kwa sababu hawana huduma yoyote ya jamii, na nimeshasema sana na wala hakuna hatua iliyochukuliwa.

Sasa ndani ya Wizara hii kuna taasisi mbili ndizo ambazo zitanifanya nisiunge mkono hoja hii. Kwanza ni Mamlaka ya Maji, watu wa Ngomeni hawana maji na nimeshasema sana, lakini hakuna *response* yoyote. Pili ni Shirika la Umeme pia nimeshasema sana na wao wenyewe wapo wananisikia, lakini kila wakipanga bajeti zao hawaweki hata jambo la kudanganyia kule Ngomeni.

Kutokana na sababu hizo Mhe. Spika, mafungu mawili haya mimi leo nazuia shilingi nasema kabisa, na wala sitakuwa rahisi hata siku moja na nilikusudia mwaka huu sitaki kuzuia kifungu chochote wala kupiga buti. Lakini Ngomeni hivi sasa mimi sithubutu kwenda, kwani nikienda kule kuna hatari hata ya kupigwa mawe kwa sababu Mwakilishi wao nipo karibu miaka 15 na hakuna ambalo wametekelezewa na serikali hii. Kwa hivyo kwa sababu hiyo, basi mimi leo nitapiga buti na nitazuia.

Nikiondoka hapo kwa haraka haraka kule Kilindi kuna miradi mitatu imefanywa. Kwanza ninamshukuru sana Mhe. Rais kwa kuahidi kuwapelekea watu wa Kilindi barabara, maji na umeme na yote *Alhamdulillah* imefanyika japo barabara ya kifusi angalau sasa gari inaweza kufika Kilindi.

Sasa jambo linalonisikitisha ni kwamba ile miradi imejengwa pale kwenye kijiji cha Kilindi tu na uwezo wa kutawanywa kwenye vijiji vyengine vya karibu upo. Kwa hiyo, naliomba sana Shirika la Umeme kupitia kwako Mhe. Spika, wasaidie kufikisha umeme katika kijiji cha Bahaani ni karibu sana.

Vile vile Mamlaka ya Maji nayo ijitahidi kufikisha maji katika vijiji vya Mtemani, Mwachawa na Kuungeni, kwa kweli ni maeneo ya karibu na kisima kile kinatosha kufikisha maji humu na wala tusibakie tu Mhe. Spika, kwa sababu ukanda wangu wote ule wa magharibi umekosa huduma kwa muda mrefu sana, sasa ikitokea huduma kama hii tusilenge kijiji kimoja. Kwa hivyo, ni vyema wajitahidi kufikisha humo angalau wawasaidie wale wananchi, kwa sababu wamekaa muda mrefu sana bila ya huduma yoyote.

Mhe. Spika, nikimaliza hilo labda niseme jambo moja tu kwenye kitabu hichi cha Mhe. Waziri ambalo linanikereketa sana kwenye ukurasa wa 21 kuna Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Kwa kweli ukisoma idara inayo mipango mizuri sana, lakini tatizo lililobakia ni utekelezaji, kwa sababu kadri tunavyokwenda ardhi yetu inamalizika, kwani mipango yetu inabakia kwenye vitabu. Kwa mfano, tunatunga sera, sheria pamoja na mipango mizuri lakini vinabakia kwenye vitabu na utekelezaji hakuna.

Mhe. Spika, tumewahi kushauri mara nyingi kwamba ardhi yetu ya Wazanzibari ni ndogo na *population* yetu ni kubwa, na sasa inakua kila siku na jamii hii inahitaji ardhi ya kulima, kuwekeza, majenzi.

Sasa mpaka leo suala hili idara hii ambayo ndio husika haijashughulikia ipasavyo, yaani mpaka leo ile ardhi ambayo inafaa kwa kilimo bado inaachiwa ijengwe majengo ya makaazi, na kuna maeneo ambayo yana ukanda mkubwa sana kwenye visiwa hivi si mazuri kwa kilimo, kwa nini serikali haielekezi majenzi kule na tukabakisha hii ardhi iliyobakia kwa kilimo.

Kwa hivyo, ukiangalia hii mipango unaikuta kwenye vitabu, lakini utekelezaji hamna kwa sababu idara hizi ndizo zinazokwenda kukata viwanja katika maeneo ambayo ni ya kilimo.

Mhe. Spika, mimi nadhani tuache hii zohali kwa sababu ardhi yetu ni ndogo, bahari inachukua ardhi kila siku na *population* inaongezeka, tutafika pahala tutashindwa hata pahala pa kupanda mbiba na itakuwa jambo la kusikitisha kweli, kwani ipo ardhi kubwa. Kwa mfano, ukienda Makunduchi kuna ukanda wa zaidi ya kilomita kadhaa hauoti kitu na wala hakuna *plan* yoyote iliyopangwa ya kujenga nyumba kule pamoja na maeneo mengine pia. Sasa kwa nini tung'ang'anie ardhi ya kilimo yote tumeshaimaliza hivi sasa.

Kutokana na hali hiyo, nafikiri watu wa Idara ya Mipango Miji na Vijiji waseme tatizo lao nini mbona hii mipango yao haitekelezeki kama ni tatizo la bajeti basi tuibane serikali wapate bajeti wafanye, lakini tukiachia hivi siku moja tutakuja kujikuta tuko pabaya kweli.

Mhe. Spika, moja katika nyenzo ya kupiga hatua ya maendeleo ya kiuchumi ni kutekeleza mipango kama hivi, kwa sababu hii mipango malengo yake ni kufikia hatua za kiuchumi na kama hatuitekelezi, halafu tutamlaumu nani kwamba sisi nchi yetu haiendelei kumbe vile ni sisi wenyewe.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Spika, nasisitiza kwamba nipate jawabu nzuri kuhusu kijiji changu cha Ngomeni kama si hivyo leo patakuwa hapatoshi hapa! Mhe. Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa ni zamu yake Mhe. Hassan Hamad Omar na baadaye Mhe. Mlinde Mabrouk Juma akifuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya, ambayo inaniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, kwa ajili ya kutoa michango yetu kwa mujibu wa kazi tulizopewa na wananchi.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu moja kwa moja niende kwenye Idara ya Nyumba ukurasa wa 30 kifungu cha 78. Kwa kweli Idara ya Nyumba imekusudia kuanzisha Sheria ya Shirika la Nyumba. Mhe. Spika, hapa niseme kwamba ninapongeza sana na ni jambo zuri la kulifanya kwa hali yote ifanikishe. Vile vile tumeambiwa kwamba tayari rasimu imeshapatikana na imeshafanyiwa majadiliano kwa Unguja na Pemba, na kwa hili niwapongeze sana. *(Makofi)*

Uanzishwaji wa Shirika la Nyumba ni zuri, kwa sababu tuangalie mafanikio ya Shirika la Nyumba ulimwenguni ikiwemo Tanzania Bara wamefika hatua kubwa sana wenzetu. Mhe. Spika, wakati nilipokuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi tulipata fursa ya kutembelea Tanzania Bara kule kwa ajili ya kujifunza, tuliona Shirika la Nyumba la Taifa limepiga hatua nzuri sana pamoja na mafanikio, wananchi wanapata makaazi yaliyo bora na salama.

Kwa hivyo, tumeambiwa rasimu hii imepata baraka za Makatibu Wakuu, basi tunaomba Makatibu Wakuu waiunge mkono na waipitishe na baadaye wailete sheria hapa tuipitishe na sisi.

Mhe. Spika, tumekwenda kule sehemu za Kigamboni kule, kwa kweli Shirika la Nyumba limejenga nyumba 200 na kabla ya kumaliza nyumba hizo basi zote tayari zimeshachukuliwa na wananchi, yaani ni nyumba nzuri ambazo ni bora tena zenye usalama. Kwa maana hiyo, hii tunaomba isizungumzwe tu kwenye kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri, isipokuwa jambo hili lifanikishwe, ili wananchi wetu wapate makaazi yaliyo bora.

Nikiondoka hapo sasa niende kwenye Mamlaka ya Mji Mkongwe. Mhe. Spika, Mji Mkongwe ni mji wa kihistoria na wageni mbali mbali hufika kwa ajili ya kujionea. Lakini kusema kweli Mamlaka ya Mji Mkongwe ni nyumba hatarishi, kwa sababu ya kuyaona hasa.

Naomba nimpongeze hapa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe, kwa sababu anafuatilia sana na wakati tulipokuwa kwenye Kamati yetu ya

Mawasiliano na Ujenzi, tulishirikiana naye vya kutosha, na alituonesha nyumba ambazo ni hatarishi na wakaazi wa nyumba ile alikuwa na matatizo makubwa, kwa sababu alipewa maelekezo na alikuwa hataki kuyafuata.

Kwa kweli kamati nayo ilifanya kazi vizuri kwa kushirikiana na Mkurugenzi huyo tukamwita na baadaye kutokana na maelekezo aliyopewa na Mkurugenzi pamoja na kamati, basi kijana huyo alitengeneza nyumba na hivi sasa iko katika hali ya salama.

Lakini *Wallahi* nathubutu kusema kwamba ndani ya Mji Mkongwe zimo nyumba ambazo ni hatari ziko nyengine zimeekewa mwega, na wakati mwengine hata kupita wale watalii wetu inakuwa ni matatizo na hali hii inakuwa hasara kubwa sana. *(Makofi)*

Vile vile ule Mji Mkongwe umependezwa na zile *tiles* za chini tu, lakini tukiangalia ndani tunafuga mapanya makubwa sana na hali hiyo inatishia amani. Mhe. Spika, naomba tuangalie kama zile nyumba zinaishi binadamu kwa sababu ziko kwenye mazingira ya hatari.

Mhe. Spika, katika Mamlaka ya Mji Mkongwe kuna wafanyabiashara hawa wanayo malalamiko makubwa dhidi ya Baraza la Manispaa pamoja na Mamlaka ya Mji Mkongwe wenyewe, kwa sababu vitu hivi vinashirikiana; wanatozwa kodi ambayo ni kubwa na wala huduma hawapati na huduma kubwa inayowapita pale ni maji, na kama maji hakuna basi biashara hizo haziko salama na sehemu zote zinakuwa ni chafu.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi atupe maelezo ya kutosha kuhusu wafanyabiashara wale, ni lini watapata huduma ya maji kwa ajili ya kuendesha biashara zao wakati kodi wanalipia na wale wanaojifanya sugu hawataki kufuata utaratibu, basi wenyewe watajua namna ya kuwachukulia hatua, lakini watu wanaolipa kodi zao na huduma zinazostahiki wapewe.

Mhe. Spika, nikienda kwenye Mamlaka ya Maji. Kwa kweli nikizungumzia maji nakusudia kwamba maji ni uhai na bila ya maji hatuwezi kuishi. Lakini jambo hili linastahiki kwa kila mtu, wanyama pamoja na baadhi ya mambo mengine tunayojifanyia sisi wenyewe na tatizo la maji limekuwa ni kubwa.

Hata hivyo, niipongeze wizara imejitahidi kufanya, lakini bado hali ni tete. Kwa mfano, tuangalie Mjini Magharibi hapa sehemu za Kikwajuni kuna matatizo makubwa ya maji na watu hawapati maji na wanachukua maji ya chumvi na hayo maji ya chumvi pia ni tabu kuyapata.

Kwa hivyo, tunaiomba wizara kupitia kwako Mhe. Spika, pamoja na juhudi zake na huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani kusema kwamba itawapelekea maji watu kwa njia ya kutumia magari, lakini isiwe ni kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa sababu matatizo ya maji yapo.

Mhe. Spika, nilipokuwa kwenye Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi pia tulipata fursa ya kutembelea katika Mamlaka ya Maji ya Arusha. Kwa kweli tumejifunza mambo mengi ikiwa ni pamoja na watu wa Mamlaka ya Maji. Sasa nadhani kama wao wenyewe kama watafanya vile wanavyofanya Mamlaka ya Maji Arusha, basi tunaweza kupiga hatua kubwa sana.

Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*) hivi sasa hairuhusu mfereji wa nje ni sawa katika udhibiti wa maji, lakini tumeona Arusha kule wenzetu kule wamejengwa kwa wale watu ambao wanaoitwa masikini wa masikini na kuwapelekea huduma ya maji, na halafu anaweza wakala wao ambaye ndiye mwenye kukusanya mapato pale. Mhe. Spika, tuliona utaratibu ule ni mzuri kwamba wawekewe na wao waweke mtu wao kwa ajili ya kukusanya mapato, lakini huduma ya maji ipatikane.

Mhe. Spika, nikiendelea kuzungumzia suala la maji, hivi juzi tu niliuliza swali langu na Mhe. Naibu Waziri alinijibu kwamba tufanye mashirikiano. Katika kijiji kinachoitwa Jitenge Maziwani Jimbo la Kojani, nilisema kwamba kijiji hichi kina matatizo ya maji na juhudi zimeshafanyika za kutosha nikiwemo mimi pamoja na Mhe. Mbunge na hata Halmashauri ya Wilaya na maji bado hayapatikani.

Kwa hivyo, tunaiomba wizara kupitia kwako Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapokuja hapa kufanya majumuisho basi anihakikishie kuwa kijiji cha Jitenge Maziwani Jimbo la Kojani ni lini kitapata maji ya uhakika na salama, na imekuwa ni tatizo sugu sana, kwa sababu sisi tumefanya mashirikiano makubwa, lakini ufumbuzi mpaka leo bado haujapatikana watu wale kupata maji ambayo safi na salama.

Mhe. Spika, licha ya matatizo ya maji yaliopo, lakini na suala la uharibifu wa mazingira katika vyanzo vyetu vya maji umekuwa ni mkubwa. Kwa mfano, ujenzi wa kiholela na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwa hivyo, tujitahidi sana katika usimamizi wetu tuliopewa majukumu ya kusimamia, na tusikae maofisini tu tukiandika kwenye makaratasi hatufanikishi. Kwa mfano, tumeona wenzetu Arusha kule wana mtandao, yaani wanazo *radio call* na wanafuatilia kila *corner* na baada ya dakika mbili tu wakipata tatizo wanakushughulikia mara moja.

Mhe. Spika, wenzetu wa *ZAWA* ndio waliotupeleka kule na wao ndio wa kulifanya hili jambo likapata mafanikio. Sasa Zanzibar bomba inaweza kupasuka hapa likachukua muda wa siku tatu bado halijashughulikiwa, huku maji yanapotea, hili ni tatizo. Tunaomba kila aliyepewa majukumu ya kufanya kazi afanye huo ndio wajibu wetu. Tunalipwa mishahara ili tujikidhi haya na wananchi tuwafanyie mema, tusiwalaumu tu wananchi tukasema kwamba ni wakorofi, hali ya kuwa wakati mwengine wakorofi tunakuwa ni sisi. Tunaiomba ZAWA ina jitihada kubwa sana kama nilivyosema, maji ni muhimu kwa kila kiumbe na mambo mengine yanayohusiana na hayo, tujitahidi sana.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende kwenye Shirika la Umeme. Kwanza niwapongeze sana kwa kukamilisha umeme ambao hauna mgao, tunashukuru. Kama kilivyoeleza kitabu hiki bado matatizo baadhi ya sehemu umeme unakatikakatika. Wametuelezea vizuri katika kitabu kwamba ni mambo ya miundombinu ambayo mengine ni chakavu. Mimi naliomba Shirika la Umeme ZECO kuwa na mashirikiano mema. Bila ya mashirikiano hamuwezi kufika popote ikiwa wengine wanafanya majungu na wengine wanafanya hivi, hamfiki na ndio inasababisha mpaka hali ikawa mbaya. Mkiwa na mashirikiano Mwenyezi Mungu anakuwa yupo pamoja na nyie, popote pale panapofanywa kazi kwa mashirikiano kwa madhumuni mema.

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba Rais wetu alizungumza kuhusu miradi ya kupeleka umeme vijijini. Mimi nashukuru sana Jimbo langu la Kojani limebahatika katika kijiji cha Kivuugo. Nina imani shughuli inaendelea vizuri na kijiji kile ni bajeti iliyopita ndio ilikuwemo sio bajeti hii tunayoipitisha leo. Namuomba Mhe. Waziri mambo yaliyobakia ni *transformer*. Wananchi wa Kivuugo walitegemea Ramadhani hii wanapata maji baridi, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi *transformer* kule haijapatikana.

Namuomba Mhe. Waziri, kufanya kitu kama hujakimaliza ni sawa sawa na kutofanya. Wanakuomba wananchi wa Kivuugo mradi ule ukamilike wa kupeleka umeme vijijini kwani nguzo zote kubwa zimeshasimamishwa bado kupelekwa *transformer tu*.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kuhusu ulinzi wa mambo yetu haya ya umeme, kuna wengine wakorofi wanazikata nyaya. Tunaiomba wizara iimarishe ulinzi, wale wasiopenda maendeleo wanazikata nyaya hizi.

Mhe. Spika, kwa mchango wangu huo mdogo naomba niishie hapo lakini Mhe. Waziri anihakikishie kwamba vijiji vya Jitenge na Maziwani ni lini watapata maji ya uhakika na Kivuugo ni lini watapandishiwa *transformer* yao

ili umeme uweze kufanya kazi zake. Kwa hayo machache nasema ahsante sana, siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo ya kuniridhisha.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa asubuhi hii ya leo kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mimi mchango wangu ni mdogo sana lakini japo mdogo tunatakiwa tutoe na hasa tukizingatia leo ni siku ya Ijumaa nitazungumza machache tu.

Mhe. Spika, mimi nazungumzia kuhusiana na Mamlaka ya Maji ZAWA, katika Jimbo la Bumbwini kwa bahati tuna visima viwili vya maji, kisima cha Makoba na kisima kilichopo Bumbwini Misufini. Kisima cha Misufini pampu ya maji imeharibika. Tunawashukuru wenzetu wa ZAWA walikuja walipoona kwamba tunakabiliwa na Ramadhani wametuletea pampu lakini pampu ile haikidhi haja. Pampu ile ni ndogo na haina uwezo, haifikishi maji kwenye tenki na maji yake hayafiki zaidi ya mita 250. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akizingatia kipindi hichi cha Mwezi wa Ramadhani watufikirie kutupatia pampu nyengine ili tuweze kukabiliana na tatizo ambalo sasa hivi linatukabili.

Mhe. Spika, pia katika Mamlaka hii hii ya Maji katika Jimbo langu kuna wafanyakazi ambao wanatumikia katika vibanda vile vya maji si chini ya miaka 12 lakini hadi hivi sasa hawajaajiriwa, hawajui hatma yao. Nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja anambie sababu zilizopelekea hadi hivi sasa hawajaajiriwa je, ni kutokana na umri, au hawana elimu au nini hasa kinachopelekea kutoajiriwa mpaka hivi sasa.

Mhe. Spika, jengine naomba nizungumze kidogo kuhusiana na Idara ya Nishati. Katika idara hii inayohusika na uchimbaji wa mafuta na mambo mengineyo. Katika mwezi wa Mei na mimi nilikuwa miongoni mwa Waheshimiwa Wawakilishi waliobahatika kwenda katika ziara ya mafunzo nchini Uholanzi. Tulipofika kule tuliona mambo mbali mbali yanayohusiana na mafuta, tunawashukuru wenzetu wale. Kati ya mambo ambayo tuliyoyaona walituonesha ni jinsi gani Zanzibar tunayo gesi ya kutosha. Hadi hivi sasa katika maelezo ya Mhe. Waziri sijaona kiasi gani kwamba tumejipanga juu ya uchimbaji wa gesi hii na mafuta.

Mhe. Spika, wenzetu walituonesha jinsi taarifa wanavyozipata kupitia *satellite* zao na wakatuonesha ukanda mzima kutoka Afrika ya Kusini mpaka Somalia, Zanzibar ndio nchi ambayo inaongoza kwa gesi nyingi. Walitwambia wakati Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano alipokwenda Uholanzi alifuatana na Mhe. Waziri wetu hapa Zanzibar na wenzetu walisema wao wapo tayari kuja kushirikiana na sisi, tuingie mikataba wafanye kazi.

Lakini walituuliza kwamba Waziri wa Zanzibar alikuja hapa na alituahidi atarudi tena, kwa sababu tulimtaka atwambie vipi kuhusiana na Zanzibar, mmejipanga vipi kuhusiana na uchimbaji wa gesi na mafuta? Walipotuona sisi walitwambia mbona Waziri hajaja? Nataka kujua Mhe. Waziri kilichomkwamisha ni kitu gani, hali ya kuwa wenzetu wapo tayari na wametuonesha mpaka aina ya meli wanayoifanyia kazi sasa hivi iko Korea, hiyo ni maalum kwa kuja kufanyia kazi Zanzibar.

Hebu Mhe. Waziri twambie tatizo ni nini? Tatizo Katiba, au tatizo hatujawa tayari? Kama tatizo ni katiba keshokutwa tunakwenda kumaliza huko. Waamuzi wakubwa ni Wazanzibari, watatoa maoni yao kuhusiana na hilo. Mhe. Waziri nikuombe sana Wazanzibari sisi ni masikini na hatuna mtaji wowote, kama rasilimali yetu ni haya mafuta basi tuharakishe. Kama wataalamu hatuna kwa kuwa mimi nilikuwa katika hiyo *Industry* ya upande wa mafuta nawafahamu kidogo Wazanzibari ambao wapo nchi mbali mbali ambao wana utaalamu wa uchimbaji wa mafuta.

Mhe. Spika, hata tulipokwenda Uholanzi tulimkuta Mzanzibari amekabidhiwa Urusi na yeye ndiye anayesimamia jinsi ya uchimbaji wa gesi na mafuta. Sasa kwa kushirikiana na hawa wafanyakazi wetu na hawa ambao tunaowaandaa kusoma mimi sioni kama tunahitaji muda sana wa kuingia hii mikataba. Niwaombe Mhe. Waziri na Wizara zinazohusika kama Wizara ya Fedha na wengine tuharakishe ili tuondokane na hili tatizo lilotukabili la umasikini ili uweze kuondoka.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia. Napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwako binafsi kwa umakini wako na umahiri wako kwa kuliongoza Baraza hili Tukufu pamoja na kutuongoza sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nitoe pongezi zangu rasmi kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano yao mazuri na uundaji wao wa mashirikiano kwa wote.

Pia nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi,Maji na Nishati kwa hotuba yake nzuri ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2013/2014. Pia nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa kuwasilisha ripoti yake nzuri ya Kamati ya Ujenzi. Baada ya pongezi hizo nianze kwanza na hii sekta ya makaazi.

Mhe. Spika, sekta hii ya makaazi ni miongoni mwa sekta muhimu kwa wananchi wetu. Kila mtu anahitaji makaazi bora na kila mtu anahitaji apate makaazi mazuri kama binaadamu wengine wanavyoishi. Nianze na suala moja muhimu sana kuhusiana na nyumba hizi za maendeleo hasa hii nyumba iliyokuwa Kengeja. Nyumba hii ipo Pemba Kengeja lakini tumekwenda kuiangalia nikiwa na mimi miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Nyumba hii nimekwenda kujionea binafsi yangu. Nyumba hii iko hali mbaya sana.

Tumeambiwa hapa katika kitabu cha bajeti kwamba inataka matengenezo ya milioni mia mbili. Hizi milioni mia mbili ni sawa sawa na kwenda kuzitia pesa baharini hazitokuwa na faida, kwa sababu nyumba hii ipo hali mbaya sana na imechoka. Wataalamu wametwambia kwamba nyumba hii tukitaka kuitengeneza tena tutumie bilioni 1.2 ndio itakuwa kwenye hali nzuri. Sasa milioni 200 na bilioni 1.2 ni vitu viwili tofauti. Lakini kwa utaalamu zaidi na wataalamu walivyosema kwamba nyumba hii ibomolewe bora ijengwe tena upya kwa sababu hali iliyokuwepo ni mbaya sana, kwa kufanyiwa matengenezo hivyo hivyo itakuwa hakuna litakalofanyika.

Mhe. Spika, nije kwenye nyumba za Michenzani za maendeleo. Nyumba hizi pia zipo kwenye hali mbaya. Namshukuru Mhe. Waziri katika ripoti yake amezungumzia kuhusu kuzifanyia matengenezo nyumba hizi za Michenzani kama kubadilisha mabomba ya maji machafu, miongoni mwa nyumba hizo ni *block* No.3. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi yake ya kuliona hilo.

Mhe. Spika, nitoe mfano pale Wete kuna nyumba moja ya Maendeleo ukiyatizama mabomba tulivyokwenda kuangalia na Kamati yako ya Mawasiliano na Ujenzi, mabomba yanavuja maji mpaka yanahatarisha usalama wa wananchi wetu. Hali ya maisha yao kiafya inaweza kuhatarika kwa maji hayo machafu kutokana na kutokuwa na usafi. Lakini nampongeza Mhe. Waziri kwa juhudi aliyoichukua katika jumba No. 3, naomba juhudi hii hii aliyoichukua naomba aichukue na kwenye nyumba ile iliyokuwepo Wete abadilishe hizi bomba kwa haraka sana. Wananchi wanasikitika sana kwa hali iliyokuwepo pale sio nzuri ya maji machafu.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri katika ujenzi wa nyumba ya maendeleo iliyokuwepo Mpapa. Sasa hivi tunavyojua, Mhe. Waziri ametwambia katika kitabu chake ujenzi unamalizika katika hatua ya mwisho. Mimi naamini uwezo tunao, tukiamua turekebishe au kujenga nyumba mpya pia uwezo huo tunao. Mfano mdogo nyumba ya Mpapa pale ni nyumba nzuri na sasa hivi ipo kwenye hatua ya mwisho inakaribia kumalizika. Naipongeza sana serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wizara yako Mhe. Waziri kwa juhudi yako kubwa uliyoichukua mpaka kuikamilisha nyumba hii.

Mhe. Spika, niingie kwenye ukusanyaji wa kodi za nyumba zetu za Maendeleo. Inasikitisha sana nyumba hizi mpaka leo mtu analipa nyumba ya Michenzani kodi shilingi elfu tisa. Hizi ni pesa kidogo sana, tuangalie hali za kodi kama vitabu vilivyoeleza kuzibadilisha hizi bei. Nimetizama kwenye Mji Mkongwe mtu analipa chumba shilingi elfu mbili mia tano. Kwa kweli hizi ni pesa kidogo sana, hata kutengeneza nyumba hizi kwa kweli haziwezi kutengenezeka. Wizara tutailamu bure, ukilinganisha na kiwango kidogo kinachokusanywa na hawa wenzetu. Kwa hivyo naomba zirekebishwe hizi kodi ili ziweze kwenda na wakati.

Mhe. Spika, Kamati yako ya Ujenzi na Mawasiliano ilikwenda kutembelea katika nyumba za NHC *National Housing* zilizopo Dar-es-Salaam. Wenzetu wamepiga hatua sana kwa nyumba zao hizi. Wanaziangalia zile kodi na wanazipitia kodi kwa kila mwaka ili kuziboresha na kupata hizi fedha ili kuweza kuzifanyia ukarabati vizuri nyumba zao ili ziende na wakati. Naomba Mhe. Spika, hili suala la kodi liangaliwe vizuri ili wananchi wetu waongeze fedha ili Idara ya Nyumba iweze kujiendesha vizuri.

Mhe. Spika, sasa niingie kwenye sekta ya maji ambayo ni sekta muhimu sana kwenye nchi yetu. Wananchi wetu wanahitaji maji safi na salama. Niipongeze sana Mamlaka ya ZAWA kwa jitihada zao kubwa ili kupata maji safi na salama baadhi ya maeneo, wanajitahidi sana.

Naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dokta Ali Muhammed Shein, Mwenyezi Mungu amuweke na ampe afya njema, kwa kubuni miradi ya maji kwa kupitia Mamlaka ya Maji kwa kubuni miradi maalum. Uchimbaji wa visima tisa vipya mjini. Hili nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa hatua hiyo waliyoiona kwa visima hivi tisa vitakavyochimbwa muda si mrefu sana.

Mhe. Spika, kwa juhudi ya serikali inajitahidi sana kuboresha miundombinu na kuweka miundombinu mipya kila siku. Kuna masikitiko kwa watendaji wetu, Mhe. Waziri hili ulione pia kwa sababu tunatengeneza miundombinu mipya, lakini kutengeneza au kupitia na kuifanyia *repair* miundombinu yetu inakuwa haina ufuatiliaji mzuri.

Mhe. Spika, tulivyokwenda Pemba na Kamati yako kutembelea kipindi cha nyuma kidogo tukafika *Airport* ya Pemba kwa kweli tukaona maji yanamwagika karibu miezi mitatu, pale *Airport*. Ukiuliza unaambiwa wizara haijatengeneza. Sasa kweli Mheshimiwa maji haya haya ndio tunayatafuta, halafu huku tunayapoteza kwa vitu ambavyo sio vya msingi na utakuta gharama zake za utengenezaji sio kubwa. Sasa tunapotengeneza hii

miundombinu tujaribu kupitia na kuifanyia *repair* sio kila siku tunatengeneza vipya, baadaye tunakuwa tunaviacha hatuvitengenezi. Mhe. Waziri naomba hilo uliangalie sana, watendaji wako wanaweza kukuharibia kwa upande mwengine.

Mhe. Waziri pia nataka nizungumzie kuhusiana na Jimbo langu la Bububu. Hivi juzi kulitiwa kifusi, mabomba yamekatwa, nasikitika sana Mhe. Waziri sisi tuna shida ya maji, lakini maji yanayomwagika pale huwezi kuamini, kutwa kucha maji yanamwagika lakini hakuna hata mtu aliyepitia kushughulikia kuhusiana na suala hilo. Ukitaka kujionea njoo utaona hasara kubwa ya maji jinsi yanavyomwagika, kuna sehemu pametiwa kifusi panaitwa kwa Handhar. Maji yanamwagika usiku na mchana mabomba yamekatika. Naomba Mhe. Waziri, ulifuatilie hili ili maji haya tunayoyatafuta tuweze kuyaenzi vizuri, tusiyaachie yakapotea bure bure.

Pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa juhudi yake kubwa ya kuuona Mjini Mkongwe kubadilisha mabomba na kutia mapya ili kuondosha upotevu huu wa maji, ili mabomba haya yaweze kuhifadhi maji vizuri na kuwafikia wananchi.

Mhe. Spika, niingie kwenye suala la malipo ya maji kwa wananchi. Maji ni tatizo kubwa na gharama zake ni kubwa, hata serikali peke yake inashindwa kuendesha. Naomba wananchi wapewe taaluma ya kulipia maji lakini kama mwananchi atapata maji na kulipia sidhani kama atashindwa kulipia suala la maji. Sasa hivi maji wananchi wengi wananunua kwa gharama kubwa. Tukitizama Mji Mkongwe sehemu kubwa maji wanapata safi na salama lakini unakuta mita hamna. Mtu anakuwa yupo yatari kulipia lakini mita hazijafika vizuri ili mtu aweze kulipia ile huduma ya maji na serikali iweze kuboresha huduma hiyo ya maji.

Mhe. Spika, naomba taaluma hii ya kulipia maji itolewe kila wakati kwenye vyombo vya habari kama TV kwenye redio nakadhalika, ili wananchi waweze kuhamasika kulipia na kuchangia sekta hii ya maji na iweze kuwasaidia wananchi waliokuwa wanyonge.

Mhe. Spika, niingie kidogo kwenye Shirila la Umeme. Kwanza nimpongeze sana Meneja wa shirika hili na watendaji wake kwa kazi yao nzito. Huduma hii ni muhimu sana katika nchi yetu. Shirila la Umeme Pemba kwa kweli linahitaji wafanyakazi wengine, wafanyakazi waliopo ni kidogo na huduma zinadhorota, Mhe. Waziri hili uliangalie ili na wao waweze kupata wenzao kuweza kusaidiana kazi zao.

Mhe. Spika, kuhusu vituo vya kuuzia umeme, mbali ukiacha Unguja lakini na Pemba hivyo hivyo wananchi wanalalamika sana kuwa vituo vipo kidogo vya kuuzia umeme. Mimi ninachosema kwa nini hivi vituo vya kuuzia umeme kwa nini visiwe masaa 24? Kwa nini sheli za mafuta zinauza masaa 24 lakini umeme mwisho saa 2 usiku. Naomba vituo vikae mpaka asubuhi ili wananchi wengine waweze kununua umeme hata nyakati za usiku ili huduma hii iweze kuwafikia vizuri wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi niseme kidogo hapa suala hili la umeme liangaliwe zaidi, wananchi wetu ni wanyonge. Siku moja mwananchi mmoja alikuwa anadaiwa na bahati mwananchi huyo alikuwa kalazwa hospitali. Basi wakaenda watu wa Shirika la umeme wakaing'oa ile mita. Yule mwananchi alikuwa hajakataa kulipa lakini alikuwa hospitali anaumwa. Wakachukua hatua ya kuing'oa moja kwa moja, hawakuchukua hatua ya kumtafuta huyu mtu na kumpa muda japo siku mbili tatu. Watu wetu kama tunavyowajua ni wanyonge na masikini, ukimwambia mtu atoe laki tatu au laki mbili sasa hivi hana, lazima afanye maarifa, akaazime, akakope ili alipe umeme kutokana na kuwa hiyo huduma kwake ni muhimu, mtu ana watoto, ana familia yake anakuta umeme umekatwa, anarudi nyumbani anakuta mita imeshaondolewa. Hili naomba tuliangalie.

Mhe. Spika, cha kusikitisha zaidi hizi taasisi za serikali hasa hii ZAWA wanadaiwa umeme pesa nyingi sana tunaweza kusema ni wadaiwa sugu, deni kubwa wanadaiwa ZAWA, unakuta deni hilo halilipwi. Wananchi wanyonge wanang'olewa mita, sasa tuliangalie vizuri Mhe. Spika, hili pamoja na taasisi za serikali, zikiwemo za Muungano na nyengine za serikali. Shirika la Umeme wataendesha shirika lao vipi kama hizi taasisi za serikali zenyewe hawalipi huu umeme. Kwanza tuiangalie serikali ilipe madeni yake halafu ndio tushuke kwa wananchi. Wananchi ni masikini, tusiwaonee sana wananchi hali ya kuwa serikali yenyewe haitaki kulipa haya madeni. Naomba taasisi za serikali ziwalipe watu wa Shirika la Umeme ili wapate kufanya kazi zao vizuri. Tusiwalaumu bure Shirika la Umeme wakati serikali yenyewe hailipi hiyo huduma. Hili naomba uliangalie Mhe. Waziri ili kuwapunguzia mzigo wenzetu wa Shirila la Umeme.

Mhe. Spika, nataka kumuuliza Mhe. Waziri je, sisi ZECO tunadaiwa na TANESCO kule Tanzania Bara, tuna madeni au hatuna madeni? Naomba kama tuna madeni tujue na kama hatuna madeni tujue. Nasikia kama tuna madeni TANESCO inadaiwa lakini hatuwezi kulipa. Kwa nini tusiweze kulipa? Naomba ufafanuzi zaidi kuhusu hili kujua madeni tunayodaiwa Tanzania Bara na wenzetu wa TANESCO.

Mhe. Spika, mimi naomba serikali iwasaidie japo ruzuku hawa Shirika la Umeme ili kuwaondoshea usumbufu mdogo mdogo ili wananchi wanyonge wa nchi hii wapate huduma hii ya umeme, ili waweze kufanya mahitaji yao kama watu wengine. Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusimama hapa. Pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii. Pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake.

Mhe. Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kuwapa pole Mhe. Waziri pamoja na wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji kwa msiba mkubwa uliotokea. Mamlaka ya Maji ilipata msiba wa kuondokewa na wafanyakazi watatu kwa siku moja. Huo ni msiba mzito, lakini kila alipangalo Mungu halipanguki. Isipokuwa sasa ni wajibu wetu kuwaomba wawe na ustahamilivu kwa msiba huo na kuwatakia marehemu Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema wenzetu waliotangulia mbele ya haki.

Mhe. Spika, baada ya kuwapa pole wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji naomba niwapongeze sana wenzetu hawa wa Mamlaka ya Maji, kwa kujitahidi kuhakikisha kama Wazanzibari wote wanapata huduma ya maji safi na salama. Ingawa bado hawajafikia asilimia mia kwani bado kuna baadhi ya vijiji vingi havijapata huduma hii. Lakini ni lazima tuwapongeze kwa sababu jitihada zao tunaziona.

Mhe. Spika, hapa nina masikitiko kidogo, mara nyingi katika mijadala yetu tunapenda sana kuwalaumu tu lakini hatuangalii maslahi yao wanayoyapata. Mafundi wa Mamlaka ya Maji wanafanya kazi kubwa na nzuri, lakini kwa kweli maslahi yao yapo chini mno. Mimi maeneo ninayoishi ni Machomane pale niko karibu na kituo cha Mamlaka ya Maji, mara nyingi huwaona mafundi wa Mamlaka ya Maji jinsi walivyokuwa hali zao za maisha ni duni mno. Kwa kweli mafundi hawa wana hali mbaya na kwa vijana wa leo huwa wana msemo wanasema wamechoka, kwa kweli wamechoka kweli kweli.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo kidogo vipi atawasaidia wafanyakazi hawa mafundi ili kuweza kupata posho maalum kwa sababu Waswahili wanasema *mcheza kwao hutunzwa.*

Suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu nyumba za maendeleo. Sote Wazanzibari hatuna budi kumpongeza muasisi wetu kwa kutuwekea nyumba hizi za maendeleo. Kiongozi wetu huyu alikuwa na fikra nzuri na muamko wa maendeleo na ndio maana akatuwekea nyumba hizi. La

kusikitisha serikali haioneshi kuzijali fikra za muasisi wetu huyu. Ukiangalia hali ya nyumba hizi zinasikitisha, ukiiona nyumba ya maendeleo iliyopo Kengeja inaliza kabisa. Naomba Mhe. Waziri aziangalie sana nyumba hizi za maendeleo zikiwemo za Machomane na Madungu, waswahili husema *'Usipoziba ufa utajenga ukuta*'**.**

Mhe. Spika, hivi sasa serikali imepanga kufanya sherehe kubwa ya kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi. Namuomba Mhe. Waziri katika kumuenzi mzee huyu basi wahakikishe wanamuenzi kivitendo, kwa kuzifanyia ukarabati nyumba zile pamoja na kuzipaka rangi. Lakini leo Mhe. Spika, tupo kwenye sherehe kama hizo kubwa yale mambo aliyoyafanya muasisi wetu hayatizamiki, kwa kweli inasikitisha.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka niligusie kidogo ni kuhusu utafiti wa uchimbaji wa mafuta na gesi. Mimi nimehuzunika sana kuona katika hotuba ya Mhe. Waziri hakuna maelezo ya utafiti wa uchimbaji wa mafuta na gesi. Kwani hivi sasa wenzetu wa Bara wanachimba gesi yao, sijui sisi Zanzibar tuna siri nini. Hapa namuomba Mhe. Waziri atakaposimama anipe maelezo mazuri.

Mhe. Spika, katika hii bajeti inaonesha kwamba serikali haina mkakati mzuri na suala hili lina ushahidi. Kwa sababu katika kiambatanisho Nam. 1(d) ukurasa wa 75. Mhe. Spika *page* hii ya 75 kiambatanisho hiki kinazungumzia wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ya muda mrefu. Katika nishati 21 na 22 pale inaonesha kama wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ni wawili tu. Hivyo kweli hapa serikali imekusudia. Mimi nilifikiria angalau serikali itasomesha kuanzia watu 20 lakini leo ni wafanyakazi wawili tu.

Je, Mhe. Waziri ikiwa hatusomeshi vijana wetu, tukiwa tayari kuchimba mafuta na gesi yetu tumekusudia tuje tutafute wataalamu kutoka jirani huku ni kutafuta kuibiwa rasilimali zetu?

Mhe. Spika, vile vile naomba niende katika ukurasa wa 85 kiambatanisho namba D3. Mhe. Spika, hapa kuna taarifa za wafanyakazi waliostaafu kazi 2012/2013. Mhe. Spika, hapa inaonesha Wizara ina wafanyakazi 2055 lakini kwa upande wa Pemba kuna wafanyakazi 195. Sasa hapa ninamuomba Mhe. Waziri anifahamishe hii ni sahihi, na ikiwa ni sahihi hii ni asilimia kumi tu ya wafanyakazi wote walioko Pemba, ninamuomba Mhe. Waziri anambie wafanyakazi hawa wanatosha kwa kule Pemba na ni sababu zipi zilizopelekea kuwa na wafanyakazi hao?

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba nije katika utumiaji wa ardhi. Nchi yetu ni visiwa na ardhi yetu ni ndogo lakini Mhe. Spika, hakuna utaratibu mzuri

wa kutumia ardhi, kwa sababu tunaona mara nyingi zile sehemu ambazo tunaweza kuzitumia kwa kilimo ndio watu wanazojenga. Na kwa hakika hii inaonesha Wizara inashiriki kwa sababu mtu hawezi kujenga kama hajapimiwa au hajapewa kibali.

Sasa Mhe. spika, hapa mimi naona huu ni utumiaji mbaya wa ardhi kwa sababu kuna sehemu ambazo pia hatuwezi kulima, lakini ziko wazi kwa nini watu wasikatiwe maeneo yale wakajenga na yale ambayo yanawezekana kulima tukalima. Mhe. Spika, hapa pia ninamuomba Mhe. Waziri anipe maelezo kwa sababu Wazanzibari wengi tunategemea kilimo na hivi sasa sehemu ambazo za kulima ndio tunazojenga majumba.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo machache ninaunga mkono hoja na ninamuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi katika masuala yangu. Ingawa kwa kuhofia kuwa sitopata kuchangia na nilipeleka mchango wangu kwa maandishi, lakini kwa vile Mhe. Spika, umenipa nafasi namuomba Mhe. Waziri anijibu.

Mhe. Spika: Ninakushukuru kwa bahati sikuwa najua kama tayari umepeleka kwa maandishi utaniwia radhi.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ninakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia hapa leo nikiwa na afya njema.

Pili napenda nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake jinsi wanavyofanya kazi ya kuihudumia jamii jambo ambalo wananchi wote wa Zanzibar wanategemea asilimia zaidi ya thamanini ya maisha yao kutoka Wizara hii.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze katika kitabu kidogo ukurasa 6 *paragraph* ya 11 kwenye uratibu na usimamizi wa Ujenzi wa Nyumba za Serikali. Hapa naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa programu yake nzuri aliyoiandaa ya kutengeneza na kufanya ukarabati baadhi ya nyumba hizi za maendeleo. Lakini Mhe. Spika, naomba nimwambie Mhe. Waziri miongoni mwa nyumba zilizokuwa za maendeleo zilizomo ndani ya hali mbaya ni nyumba za maendeleo za Wete, zile nyumba zina hali mbaya sana, ni hatari hasa kwa maisha ya watu, sasa ninamuomba Mhe. Waziri na katika programu zake zote nilizoziomba sijapata kuona sehemu yoyote ambayo inazungumzia angalau kufanyiwa ukarabati kwa nyumba zile za Wete.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe.Waziri atakapokuja hapa anipe maelezo angalau ni lini nyumba zile nazo zitafanyiwa ukarabati zionekane angalau zinasimama vizuri katika kuyaenzi matunda ya muasisi wetu wa nchi hii.

Pili Mhe. Spika, naomba niingie katika programu ya usambazaji maji inayofadhiliwa na ADB, programu hii Mhe. Spika, inakwenda kwa kusuasua sana hasa katika maeneo ya mji wa Wete, na pia katika programu hii hakuna utaratibu mzuri wa kutathmini vipando vya watu. Mhe. Spika, hapa utakuta miti tu inakatwakatwa ovyo ovyo bila ya wenyewe kupewa taarifa na wanapoulizia wanaambiwa hapa panapita pampu za maji. Sasa ni kweli maji ni muhimu, maji ni maisha ya kila mtu na kila mmoja anataka maendeleo. Lakini kwa nini basi angalau wale wenyewe hawawapi taarifa mapema wakakubaliana kwa sababu maji ni maendeleo lakini pia na mikarafuu ni mali ya taifa.

Kwa hivyo kama kuingia tu na kukatakata ovyo hii miti bila ya wenyewe kupata taarifa wala hakuna malipo ni hatari Mhe. Waziri. Kwa hivyo ninakuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa utupe ufafanuzi hasa ni kitu gani kinachosababisha watu hawa kuingia tu na kukatakata ovyo ovyo bila ya kuwapa wenyewe taarifa sahihi.

Mhe. Spika, naomba nije katika Mamlaka ya Maji; niko katika mradi wa usambazaji maji. Kama ninavyosema maji ni uhai ninamshukuru sana na ninaipongeza sana Wizara hii kwa jitihada zake za kueneza maji mijini na vijijini Unguja na Pemba. Nataka niwapongeze sana kwa jitihada zao hizi lakini bado kuna maeneo mengine yanatakiwa yapewe kipaumbele Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri Uvinje ndani ya Jimbo la Gando Wilaya ya Wete ni kisiwa, kisiwa hiki kina wakaazi wasiopungua 400. Sasa watu hawa Mwenyezi Mungu aliwajalia wakabahatika kupata maji mwaka 2004 kupitia mradi wa TASAF. Pesa nyingi zilitumika katika kupata maji kwenye Kisiwa hiki, zilitumika kama sikosei karibu milioni hamsini. Wenyewe walichangia na wafadhili mbali mbali na kupitia Wizara hii pia ilifanya jitihada kubwa lazima tuipongeze.

Lakini sasa Mhe. Spika, karibu miaka miwili na nusu wanawake wa kijiji kile au wananchi wanaoishi kutoka kisiwa kile cha Uvinje hawapati maji. Wamerudia tena kazi yao ya kwenda kufuata maji Wete kwa mitumbwi jambo ambalo ni hatari kwa maisha watu wa ndani ya kisiwa kile.

Kwa hivyo katika hili ninamuomba Mhe. Waziri alisimamie sawa sawa mimi sina tatizo na kupitisha bajeti lakini likifika hili kama sijapata uthibitisho wa

dhati kabisa kwa watu hawa kupata maji watu wa Kisiwa cha Uvinje basi nitazuia fungu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, matatizo ya ndani ya visiwa kila mmoja anaelewa. Kama wazanzibari wengi tulipoteza maisha kwa sababu ya meli, baada ya hilo jitihada za serikali zimeonekana na meli iko njiani, lakini je sasa na hawa watu wa Uvinje uwatie baharini kwa sababu ya kwenda kutafuta maji Wete ndio tuangalie programu hii ya kufufua angalau ile miradi iliyomo mule ya kupatikana maji.

Ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniambie ni lini wananchi wanaoishi katika Kisiwa cha Uvinje wasiopungua 400 waliopata maji kwa thamani kubwa na pesa nyingi zilizopotea za serikali leo watapata maji yale, lini angalau na wao kunusuru maisha yao katika bahari katika kuvusha maji katika Mitumbwi.

Mhe. Spika, kidogo nataka niingie kwenye suala la migogoro ya ardhi. Migogoro ya Ardhi Mahkama za Ardhi zipo, kesi zinakwenda katika viambatanisho vyake tumeelezwa kuna kesi ngapi, ngapi zimepatiwa ufumbuzi lakini nataka niseme Mhe. Spika, suala hili ni gumu na lina kazi na linahitaji uangalifu wa hali ya juu. Kwani kuna baadhi ya watu wamejitokeza wanauza viwanja kiwanja kimoja anaweza akauziwa mtu au wakauziwa watu sio mtu. Anaweza akauziwa mwengine leo, kesho akauziwa mwengine, keshokutwa mwengine.

Kwa hivyo ninaiomba Wizara sana ilisimamie hili ili kupunguza hii migogoro ya ardhi, kwa sababu baadhi ya migogoro ya ardhi inakuwa katika hali kama hiyo. Mtu anatoa pesa ananunua kiwanja leo kesho anauziwa mtu mwengine, keshaanza kujenga anaambiwa hili na hili na ukienda mahkamani kesi inakuwa kubwa inachukua muda mrefu mpaka watu wanakata tamaa. Kwa hivyo ninakuomba sana Mhe.Waziri ulisimimie kwa nguvu zako zote na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atakusaidia. Na ninavyokujua kwa utendaji wako basi hili utalisimamia vizuri.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa sababu sitaki nichukue muda wako mwingi niwakoseshe wengine nafasi, nataka nimalizie kidogo kwenye uchimbaji wa mafuta na gesi. Mhe. Spika, nchi yetu ni maskini tunayoiona lakini nchi yetu ni tajiri sana. Wengi wameshasema wanaojua mambo ya utaalamu waliokwisha kutembea katika sehemu na wakaona jinsi ya mambo yalivyo. Lakini hapa kwetu katika hotuba hii sijawahi kuona eneo linalozungumzia mambo ya uchimbaji wa mafuta na gesi.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri matatizo yote yaliyomo ndani ya Wizara yetu hii na serikali kwa jumla yataondoka pindipo tu tukianza kutafuta hii raslimali yetu tuliyonayo kuchimba, na hapa itakuwa hakuna mwenye tatizo la maji, hakuna atakayelipia elimu, hakuna atakayelipia afya na mambo mengine.

Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Waziri katika hili atakapokuja atupe ufafanuzi kidogo angalau tujenge matumaini katika hili.

Baada ya kumaliza hayo nitaunga mkono hoja baada ya kuhakikishiwa ni lini watu wa kisiwa cha Uvinje watapata maji, na lini nyumba za maendeleo zilizoko Wete zitapatiwa angalau ukarabati kuonekana na ule mradi ulioko kule Wete kwa watu wanaon'golewa vitu vyao ovyo bila ya kupewa taarifa.

Ninakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru na mimi kunipa nafasi hii nikazungumza machache sana katika Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mhe. Spika, nataka niendelee kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuweza kutuhudumia sisi wananchi wa Zanzibar.

Baada ya hayo sasa moja kwa moja nataka nianze na mchango wangu. Mhe. Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja katika maeneo ambayo bado yananipa tabu kuendelea kuunga mkono bajeti hii, na baadae nitakuja yale mengine ambayo nitajaribu sana kuishauri Wizara.

Mhe. Spika, nimejaribu kuangalia kitabu cha Mhe. Waziri sikuona utekelezaji wa ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi hasa kuhusu suala la mambo yaliyobainika katika Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, tunatambua kwamba Shirika la Umeme lina watendaji wazuri, waadilifu na wanajitahidi kuchapa kazi. Lakini kwa kuwa kuna baadhi ya mambo yalionekana mimi nadhani ilikuwa ni busara tungelipata maelezo ili na sisi tukaweza kujiridhisha kwamba kweli serikali yetu kwamba kwa yale maeneo ambayo hayafanyi vizuri basi kuna hatua vile vile za kisheria zinachukuliwa.

Sasa Mhe. Spika, mimi katika eneo hili kwa kweli nitakuja kuzuia fungu mpaka nipate maelezo ya kutosha kabisa. Na Mhe. Spika, kama nitakuwa sijapata maelezo ya kutosha basi nitajaribu kuangalia ni eneo gani ambalo nitakaloweza kuondoa shilingi mia katika mshahara wa Mhe. Waziri, na ninaamini nikiweza kuondoa shilingi mia katika mshahara wa Mhe. Waziri

basi naamini ataacha shughuli zake zote ili kuja kuturidhisha kwa jawabu ambazo zitakazoweza kuwaridhisha na Wajumbe wenzangu wengine.

Lakini jengine kitu ambacho ninachotaka kukisema kwamba pamoja na hayo Shirika la Umeme tunajua majukumu mazito waliyokuwa nayo, na tunashukuru sana sasa hivi alau wameanza kidogo kujirekebisha. Mimi niseme kelele ndio kazi yetu hapa baada ya kelele kidogo za muda mrefu tunahisi kuna baadhi ya mambo yanaanza kurekebishwa. Kwa hivyo tunaomba uendelee na moyo huo huo wa kuweza kuwatumikia wananchi wetu.

Sasa nikiondoka hapo Mhe. Spika, nataka nije katika eneo jengine ambalo pia nitakuja kuzuia fungu kama sikupata maelezo ya kina na ya kutosha katika eneo la Mamlaka ya Maji. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametuomba fedha nyingi sana katika miradi ambayo iliombewa fedha nyingi katika serikali kwa mwaka huu ni mradi wa maji, ambao karibu zaidi ya bilioni hamsini na tano zimeombwa na Mhe. Waziri nataka kuziruhusu tumwachie ili aende akatumie kwa ajili ya kuwaletea huduma za maji.

Lakini Mhe. Spika, mimi hapa Barazani si mgeni tumeshaombwa mafungu kama mara nyingi na Idara hii ya Maji tokea ilipokuwa Idara na mpaka sasa Mamlaka ya Maji. Mhe. Spika, nitakuja kuhitaji maelezo ya kina kutoka kwa Mhe. Waziri ni namna gani kiasi cha fedha ambacho tulichokitumia kwa ajili ya mradi wa Japan wa Mkoa wa Mjini Magharibi, na ni asilimia ngapi ya mafanikio tuliyoyatarajia tumeweza kufanikiwa. Vyenginevyo Mhe, fungu hili ninaweza nikaleta tabu kidogo katika kuliruhusu kwa sababu isiwe kila siku tunapitisha fedha, na hizi fedha Mheshimiwa halafu ndio inakuja kama deni la taifa. Sasa huu mzigo baadae unakuja unakuwa ni mzigo wa wananchi.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhan tunashukuru tumesikia Mamlaka ya Maji watatutembezea magari ya maji, lakini Mheshimiwa ni sawa sawa na kumpa mtoto kinyonyo. Mimi nadhani watusaidie kujenga miundombinu hasa ile ambayo tuliyoianzisha sisi katika majimbo yetu. Mfano Mhe. Spika, sasa hivi katika eneo ambalo linatuumiza sana tumepewa fedha sisi za miradi ya maendeleo na serikali tunaishukuru sana serikali yetu, fedha zile bado tumeendelea kuwapa Mamlaka ya Maji maana ya ukiacha hii bajeti ambayo wanaiomba na hizi fedha na zile tulizopewa na serikali bado tunazipeleka kule kule Mamlaka ya Maji.

Kwa sababu kwa kuwa wao wameshindwa kutuletea maji kwa wananchi wetu inabidi tuchimbe visima, hivi sasa hivi ukienda Kwamtipura Mheshimiwa mafundi wapo wanaendelea kufanya kazi. Sasa mimi naomba sana badala ya kuniletea magari ya maji mimi nileteeni matenki ya maji, nileteeni Simtank za

maji na kuchimba visima ili wananchi wangu wapate maji. Kwa sababu ukinileteа gari la maji, leo ikimaliza Ramadhani haya utaniletea tena gari la maji, lakini ukinileteа Simtank la maji nikiweka pale juu wananchi wangu wa Kamtipura wataendelea kunywa maji kwa kupitia nguvu za Mwakilishi wao mpaka pale serikali mtakapokuwa tayari kutuletea maji. Sasa Mhe. Spika, sitaki kusema kwamba wananchi wangu wasipelekewe maji, lakini hili ndio wazo langu sitaki mnipe kinyonyo, mimi nataka mnipe mshipi nikavue samaki Kwamtipura. Sasa Mhe. Spika, hiyo ndio hoja yangu katika Mamlaka ya Maji baada ya kupata maelezo hayo mengine yatafuata baadae.

Mhe. Spika, nikiendelea katika mchango wangu kuna suala la ujenzi wa nyumba.Mimi nitaendelea kusema, nimeshasema na nitaendelea kusema, yale madhumuni au malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo muasisi wetu Mzee Abeid Amani Karume, moja katika malengo yake ni kuwapatia makaazi bora wananchi wa Zanzibar. Mhe. Spika, ni aibu, hebu leo *imagine* ivute picha ya miaka ya 72 angalia na nyumba zile za Michenzani, vuta ile fikra yako ilete nyumba zile ziko katika miaka ya 72, sio ya sasa hivi wananchi washakuwa na uwezo wa kujenga ghorofa wenyewe, enzi zile serikali iliweza kujenga nyumba, kuna watu walikuwa wanatoka shamba wanakuja mjini kuja kuangalia nyumba za Michenzani. Leo kaondoka Mzee Karume na nyumba zimekwama pale pale.

Mhe. Spika, sasa hivi kuna mambo ya kidunia, serikali nyinyi hamna haja nyinyi kutoa pesa mfukoni. Mimi nadhani nimeshazungumza na nitazungumza. Kuna wafadhili ambao wana fedha taslim, serikali iseme tu kwa ajili ya kujenga nyumba mpaka leo huko kimya.

Sasa Mheshimiwa hili suala nilimwambia Makamu wa Pili wa Rais, sasa hivi ninamwambia mwenyewe muhusika Mhe. Waziri wa Ardhi,Maji, Makaazi na Nishati Mheshimiwa wafadhili hao wapo, nilikwambieni hapa mkanambia mtanitaka nikutapatieni *e-mail* yake, baada ya kuondoka hapa kila mmoja ana shughuli nyingi na mimi nimenyamaza kimya ninakusubirini.

Sasa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amealikwa na hao wafadhili wenye hiyo miradi ya ujenzi wa nyumba, sasa naomba kama Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hatopata safari ya kwenda huko Marekani, Mhe. Waziri aende yeye na watendaji wake wa Idara ya Nyumba Ardhi na vitu vyengine. Kule Mheshimiwa atakwenda kukutana na hao wafadhili ambao wanataka kuja kuwekeza katika miradi ya nyumba.

Mhe. Spika, ninaamini Mhe. Waziri atakuja kunipa maelezo ya kutosha katika hili, tunahitaji wananchi wetu wapate makaazi ya kutosha.

Mheshimiwa Zanzibar katika nchi ambayo nzuri duniani kutokana na jiografia yake na mazingira yake ni Zanzibar, lakini hatujaijenga. Mhe. Spika, sawasawa samahani kidogo mwezi wa Ramadhani lakini nitatoa mfano si mbaya sana. Mfano mwanamke ukimkuta katika hali ya kawaida baada ya saa 2.00 ukamkuta ameshajipodoa hali itakuwa vipi? Inakuwa tofauti na ndio maana wazee wetu wanatwambia kama unataka kuchagua mke usichague siku za sikukuu, kwa sababu gani anakwenda anarembwa rembwa. Zanzibar kisiwa chetu hatujakiremba, Mheshimiwa Zanzibar yenyewe hiki kisiwa kinajiuza.

Mhe. Spika, najua unaniangalia angalia muda wako siku hizi unakuwa umejibana sana, kwa hivyo mimi naamini tena basi Mhe. Spika, hivi juzi katika ziara ya Rais Obama, huyu muwekezaji alikuwa katika msafara ule, akatuuliza mbona *e-mail* sijajibiwa, yaani Mhe. Spika, sijui tunataka nini. Sisi tunakwenda huko nje kutafuta watu wanakuja wenyewe tunashindwa kuwafuata. Mhe. Spika, hili naomba sana Mhe. Waziri na kama atahitaji leo leo nitampatia *contact* za huyo mtu na hiyo safari ninafikiri kama atakuwa hakujui mimi nitampeleka.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakuja katika eneo hilo hilo bado niko katika maeneo ya majenzi. Mheshimiwa tumetoa viwanja maeneo mbali mbali lakini tatizo natoa mfano kama mfano Tunguu. Vimetolewa viwanja lakini vimetolewa viwanja mwituni. Kwa nini serikali isiweke utaratibu Wizara ya Ardhi inayopima viwanja kwa kushirikina na Wizara ya Miundombinu *at least* wakaweza kutoa zile njia za mwanzo kuweka zile *block at least* maana yake kuwafanya wananchi wawe na *speed* vile vile ya kuweza kujenga hizo nyumba zao.

Mhe. Spika, nataka nije katika Idara ya Ardhi, katika eneo hili Mhe. Spika, nitaomba uje uniruhusu nizuie sana mafungu nipate maelezo kwanza kuna wananchi wa Nungwi, wananchi hawa wa Nungwi Mhe. Spika, waliwahi kuombwa na Rais mstaafu Dr. Salmin Amour Rais wa Awamu ya Tano waliombwa eneo lao wairuhusu serikali ijenge *rest house*. Lakini kwa bahati mbaya muda mrefu umepita awamu ya tano imepita, awamu ya sita imepita *rest house*, Dr. Salmin mwenyewe akatoa barua wale wananchi baada ya kwenda kulalamika wanataka kutumia lile eneo lao, Dr. Salmin aliandika barua na kopi nnazo akawapelekea serikali kwa kutaka kwamba lile eneo kwa kuwa ile *rest house* ya Ikulu haikuwahi kujengwa warejeshewe wenyewe.

Mhe. Spika, ninaishukuru sana serikali pale kuna familia mbili, Familia moja wamepewa eneo lao lakini familia ya pili mpaka leo hawajapewa eneo lao. Sasa Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri itabidi aje anipe maelezo ya kutosha.

Lakini jengine Mhe. Spika, tulipokuwa tukifanya kazi ambazo umetutuma kushughulikia masuala ya matatizo ya wananchi tulikwenda Paje. Paje kuna mwananchi pale Mzalendo tumekwenda mpaka na watu wa ardhi hili suala wanalijua naamini watakuja kunipa maelezo ya kutosha. Lakini sio maelezo ya mdomo nataka maelezo ya kutatua tatizo hili.

Mhe. spika, kuna mwananchi mzalendo analo eneo lake pale liko Paje, eneo lile alipokuwa anataka kujenga kuna muwekezaji wa hoteli pale inaitwa *Cristal* mbabe, huyo maana yake watu wa Paje wote wanamwita mbabe muwekezaji wa Kampuni ya *Cristal*, amelichukua eneo lake amemzuia asiweze kulitumia hilo eneo tena ndani ya hilo eneo huyo muwekezaji amejenga vinyumba vya kulaza wageni ndani ya eneo la mzalendo hii haki? Hii jamani watendaji wetu wa serikali wapo? Wananchi wa Zanzibar wananyanyaswa ndani ya ardhi yao na wageni.

Mimi ninafikiri kama hizi kazi zimeshakushindeni hebu rejesheni hizo kalamu za watu huko ofisini wapewe watu wengine. Mhe. Spika, naomba sana huyu kijana Ndugu Mudrik ameshakula hasara sana ameleta maboti yamefika pahali yameoza, serikali ipo inamuangalia eneo lake linatumiwa na mtu mwengine bila ya kuweza kupatiwa haki zake. Na hili nitaomba maelezo.

Lakini jengine kuna muwekezaji ambaye huyu ameshaanza kuwekeza kuna Kampuni wanaita *Zan Recreational Product limited* hawa Mhe. Spika, wanafanya shughuli za *air craft* mambo ya kufundisha marubani. Mhe. Spika, muwekezaji huyu sisi tulipounda Kamati Teule ile ya mwanzo kabisa tulikwenda katika eneo lake pale tukajaribu kumuona amekodi kuna henga pale la Mkurugenzi mmoja wa Serikali, kuna henga pale uwanja wa ndege amekodi na anaweka ndege zake kipindi kile tulichokwenda sisi Mhe. Spika, alikuwa ameshawekeza ndege mbili. Sasa hivi ameongeza ndege nyengine ndege nne. Huyu ameomba eneo katika eneo la Kigunda, Kigunda ninafikiri Mkwajuni, Mheshimiwa Naibu Waziri anatikisa kichwa analijua.

Eneo hili Mheshimiwa ameona kujibanabana hapa uwanja wa ndege wa Zanzibar ameona atafute eneo na *document* za serikali ninazo hapa, *document* za ZIPA kila kitu amesharuhusiwa kuwekeza mradi wake wa kujenga kiwanja kidogo cha ndege cha kufundishia marubani, na sasa hivi keshafundisha marubani karibu 55. Katika marubani hao 55 marubani 32 ni Wazanzibari wakaazi, leo tunamzuia mpaka leo asiweze kuwekeza ameambiwa atafute eneo, katafuta eneo ameshawalipa wananchi fidia sasa hivi kuna tatizo gani.

Mhe. Spika, muwekezaji huyu kuna na wenzake vile vile wametaka kuja kuwekeza hapa Zanzibar, lakini tokea mwaka 2009 alipoanzisha mradi wake mpaka leo tuna mwaka 2013 anapigwa dana dana, leo muwekezaji gani

mwengine atakayeweza kumshawishi akaja? Mimi naomba Mhe. Spika, kama hakuna tatizo lolote la kiusalama wa nchi basi aruhusiwe mzalendo huyu aweze kuwekeza ili vijana wetu wengi wa Kizanzibari waweze kupata kazi za urubani.

Mhe. Spika, kama tunavyozungumza ajira ngumu, lakini hawa vijana 50 aliowasomesha wa Kizanzibari wote sasa hivi wako angani wanapishana wanarusha ndege. Sasa leo huyu akiweza kupata hiki kiwanja Mhe. Spika, akiweza kuruhusiwa kujenga hiki kiwanja cha ndege kidogo katika eneo la Kigunda ataweza kurusha ndege, tena kwa bahati nzuri Mheshimiwa katika hizo ndege nne alizoleta zina uwezo mpaka wa kutua baharini. Leo Mhe. Spika, nchi yetu hii nchi ya Visiwa, siku zote mameli Mungu apishie mbali yanazama, viboti vinazama, tunaweza tukatumia hata hizi ndege zake kwa kwenda kuokoa watu zinatua mpaka baharini.

Ameleta vifaa vya kutua ndege baharini, ameshindwa hajapewa ruhusa ya kuweza kuvitumia, ameng'oa vifaa vile ameviweka pembeni. Jamani kweli hii nchi ya visiwa Mheshimiwa, kweli tuko *serious* katika uwekezaji. Nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, kama hakuna sababu za kimsingi basi aruhusiwe muwekezaji huyu aweze kujenga hiki kiwanja kidogo cha kurushia ndege, ili kuweza kutoa taaluma kwa wananchi wetu mbali mbali.

Mhe. Spika, najua bado dakika tano, sasa Mhe. Spika, nilikuwa naulizia vile vile kuna Mheshimiwa huyu mwenzetu ambaye kakitumikia chombo hiki kwa muda mrefu, hatupendi kuombeana sisi Waheshimiwa lakini mwenzetu sasa hivi ameshatoka humu Barazani Mhe. Kamal.

Mhe. Spika, eneo la pale Darajani eneo lile kwa muda mrefu mimi mwenyewe aliniita nyumbani kwake akanisikitikia sawa alitaka kujenga kituo cha Petroli pale haiwezekani basi ata nyumba au akajenga mradi wowote wa kufanya biashara. Kitu ambacho anachosikitika wenzake kwa nini wanapewa katika eneo lile wanajenga yeye azuiwe mpaka leo. Mhe. Spika, yule mwenzetu tusimzeeshe mapema naomba sana Mhe. Waziri tena ninajua Mheshimiwa Waziri aliwahi kuwa Waziri mwenzake hebu ampe ile haki yake ili aweze kuitumia kwa kulijenga lile eneo lake.

Mhe. Spika, jengine nililokuwa nataka nilizunguze suala la hati miliki ya miradi yangu ya Jimbo langu la Kwamtipura. Hili Mheshimiwa ninajua watendaji wanalijua vizuri naamini watampa maelezo ya kutosha akija atakuja kunijibu ili niweze kumruhusu kuendelea na mambo mengine.

Lakini jengine Mhe. Spika, nilikuwa nataka nizungumzie suala hili ambalo Mhe. Waziri nataka niseme amelionea haya kulizungumza au kuliingiza

katika kitabu chake. Suala la utafutaji wa raslimali ya mafuta na gesi katika Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nadhani wakati umefika, wakati umefika hali ngumu ya uchumi wananchi hali zao si nzuri, na kwa kuwa wananchi wameshaambiwa kuna raslimali ipo, serikali haina majibu mpala leo wananchi watatuelewa vipi hebu tuambiwe. Mimi ninafikiri Mhe. Mlinde kafanya kazi nzuri sana maana mpaka Waziri anaulizwa Uholanzi huyu Waziri atakuja lini? Mhe. Spika, wenzetu tunaona wanapishana wawekezaji wanakuja sisi raslimali tuliyokuwa nayo Mhe. Spika, sisi ndio watunga sheria kama kuna matatizo ya kisheria tuletewe mswada hapo wa sheria tuweze kurekebisha ili hili suala tena liweze kukamilika.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache mpaka sasa hivi kwanza nina asilimia thalathini ya kuunga mkono Wizara halafu baadae asilimia sabiini. Naamini Mhe. Waziri, atakuja na jawabu za kutosha naamini nitaweza kuachia fungu hilo kwa niaba ya wananchi wa Kwamtipura, na wengine wale walionituma ambao hawaishi Kwamtipura. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru mchana huu kupata fursa ya kusema machache katika mchango huu wa Wizara ya Maji, Nishati na Ardhi. Kwanza Mhe. Spika, najua kwamba Wizara hii inamgusa kila raia, na Waziri katika kujibu masuala mbali mbali ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi aliahidi kwamba katika mwezi huu wa Ramadhani atajaribu kusambaza maji kwa wale ambao hawayapati.

Mhe. Spika, ninachokijua ni kwamba wengi hatupati maji, sasa sijui hili zoezi limeshaanza na kama limeshaanza limeanza katika Shehia zipi na labda litaenea kwa nchi nzima. Nasema hivi kwa sababu utaratibu uliopita ulikuwa ni kuwasaidia zaidi wananchi waliokuwa katika maeneo ya mijini, kwa wale walioko vijijini hawaipati huduma hii, sasa je mara hii na wale ambao wako vijijini hawapati huduma hii watapatiwa au tutaendelea kuwapatia wale wale wa mjini tu.

Mhe. Spika, Mhe. Ussi wa Jimbo la Chaani, alipoanza kutoa mchango wake alisema ataondoa shilingi na Mhe.Abdalla Juma, wa Jimbo la Chonga na yeye vile vile alisema ataondoa shilingi na sababu yao kubwa ni kwamba Mhe. Rais, katika ahadi zake ni kwamba katika sehemu zao basi watapatiwa huduma hii muhimu ya maji pia na umeme. Na mimi niseme tu kwa vile wao wameshatosheleza kuondoa shilingi mimi sitaki niiondoe, lakini nimkumbushe Waziri kwamba katika ahadi alizozitoa za kuwapatia wananchi maji salama pamoja na umeme ni pamoja na kisiwa cha Makoongwe.

Mhe. Spika, nafikiri tunafahamu kwamba mazingira ya visiwa kunakuwa mara nyingi kuna majabali kwa hiyo upatikanaji wa maji ni mgumu sana. Nashukuru kwamba utaratibu uliandaliwa na hivi sasa kwa asilimia chache wananchi wameshaanza kuyapata maji, lakini bado hayajatosheleza na imekuwa ni usumbufu kwao. Kwa hiyo ningeomba ile ahadi ya kuwapatia maji pamoja na umeme ikatekelezwa.

Mhe. Spika, wengi waliozungumza hapa waligusia migogoro ya ardhi, na nakumbuka kwamba Baraza lako tukufu katika kipindi cha bajeti iliyopita liliteua kamati maalum kwa ajili ya kushughulikia suala hili na kuleta ripoti. Hii inamaanisha kwamba migogoro ya ardhi ni mikubwa na mingi katika nchi yetu. Lakini la kujiuliza kwa nini migogoro hii kila leo inaendelea na kila leo ikiendelea haipatiwi ufumbuzi?
Migogoro hii Mhe. Spika, huwa inamalizia Mahakamani, lakini kila nikiangalia kwamba Mahakama zilizopewa kazi ya kuitatua migogoro ya ardhi ni kidogo na pia mbali na udogo huo vitendea kazi hawana, unaweza kukutia Pemba nzima kuna Mahakama pengine moja tu ambayo hata usafiri haina.

Ninachokijua ni kwamba migogoro hii ipo vijijini zaidi, kwa hiyo ufuatialiaji wake unahitaji usafiri, ningeombaWizara ikaliona hilo, kwa vile migogoro imejaa katika nchi yetu basi ikaona iipe umuhimu wa kutanua hizi Mahakama zikawa zinapatikana kila pahali ili labda kurahisisha suluhu zipatikane kwa haraka pamoja na kuwapatia vitendea kazi vya kileo.

Mhe. Spika, kwa muda mfupi ambao nilikuwa katika kamati hii au bado ninaendelea nayo, nimegundua kwamba elimu tuliyonayo jinsi ya umiliki wa ardhi ni ndogo, hivyo ningewaombaWizara wakachukua juhudi za makusudi ili kuelimisha wananchi jinsi gani ya umiliki wa ardhi. Bado tunaendelea na mawazo ya kuona kwamba babu yangu alikuwa anaishi hapa au sisi tulikuwa tunazikana hapa kwa hiyo tayari sisi kwa vile babu alizikwa hapa umiliki wa ardhi ile itakuwa ni wa babu yetu. Hivyo Wizara inahitajika hivi sasa kutoa taaluma ya kutosha ya kuwaelimisha wananchi ili wajue umiliki wa ardhi uko wa aina ngapi na uko vipi. Nadhani kwamba tukifanya hivyo basi baadhi ya migogoro itaondoka.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende kidogo katika nyumba za maendeleo. Wengi wamesema hapa kwamba lengo lilikuwa ni kuwapatia wananchi nyumba bora tukijua kwamba wengi tumehangaika ili kuweka nchi iwe huru, sasa faida zake ni kuwapatia wananchi makao mazuri.

Mhe. Spika, sijui kuna utaratibu gani, lakini hivi sasa kuna baadhi ya nyumba ambazo huwa naziona tayari zimepigwa mnada au zimeuzwa na nyengine

wameshanunua raia wa nchi hii. Sasa je ile sheria inasemaje kuhusu nyumba hizi za maendeleo, kuna baadhi zinauzwa baadhi haziuzwi na kama zinauzwa kuna taratibu gani zinazotumika ili nyumba hizi ziuzwe kwa raia wetu.

Mhe. Spika, sasa niende katika nyumba za Serikali. Sijui tuna idadi maalum Mhe. Waziri, takwimu inayotuonesha kwamba hivi sasa Serikali ina nyumba ngapi na ziko katika maeneo gani, lakini la ziada ni kwamba kuna utaratibu wa watendaji wetu kuwapatia nyumba, pengine unapokuwa Katibu Mkuu au unapokuwa Waziri. Lakini Mhe. Spika, cha kushangaza ni kwamba kiongozi yule anapomaliza muda wake kutumikia Serikali anakuwa haondoki au hahami katika nyumba ile na baadae anaendelea kuihodhi.

Sasa mimi ningeuliza je taratibu na sheria zinasemaje na kama wanaendelea kuhodhi tukawaacha wale walioko hivi sasa wakaendelea kukodishwa majumba kwa fedha za Serikali hatuoni kwamba hilo si jambo zuri, wale ambao muda wao umeondoka kwa nini hatuwaondoi na tukawapatia wale ambao hivi sasa wapo katika madaraka.

Mhe. Spika, ni mara nyingi huwa tunazungumza na bajeti iliyopita ilizungumza sana kuhusu nishati mbadala, na kwa kumbukumbu zangu ilitaja kwamba imefanya utafiti katika baadhi ya maeneo ya Nungwi, Matemwe na sehemu za Pemba. Nilikuwa na mawazo kwamba kwa vile utafiti umeshasema kwamba eneo hili lina uwezekano wa kupata nishati mbadala basi tuendelee kulifanyia maendeleo mengine, lakini hadi tupo hapa hivi sasa bado tunaendelea kuambiwa tena kwamba tutafanya utafiti ili kuona nishati gani mbadala iweze kutumika katika nchi yetu.

Nafikiri Serikali imesahau kwamba nishati ya umeme tunayoitumia hivi sasa ni nishati ya kubahatisha, kubahatisha kwa maana huko tunakopewa huo umeme inategemea tabia nchi, na nafikiri historia inafundisha kwamba kwa muda wa miaka mitatu iliyopita ilikuwa mabwawa ya Mtera hayana maji ya kutosha na ilibidi tuendelee kupata umeme wa mgao, nashukuru kwamba hiyo *cable* iliyozamishwa ina uwezo mkubwa, lakini uwezo wake wote utategemea mvua imenyesha kiasi gani. Sasa mimi nahisi Wizara ingelijua hilo kwamba hivi sasa kuendelea kutumia umeme ule ni *risk*, tunahitaji tufanye maendeleo ya haraka katika kupata umeme mbadala.

Mhe. Spika, narudi tena katika sekta ya maji. Mheshimiwa aliyenitangulia alizungumza sana na akasema kwamba kuna mabilioni ya pesa yanayoingizwa katika kuendeleza au kutafuta upatikanaji wa maji safi na salama. 2010/11 Mhe. Spika, karibu bilioni kumi na nane zilitumika katika upatikanaji wa maji baada ya kuchimba visima vilioko Kijichi pamoja na Welezo. Na kwa muda wa karibu miezi mitano, sita maji yalikuwa

yanapatikana, lakini la kushangaza Mhe.Spika, maeneo yale yale muda wa miezi yalikuwa yanapata maji hivi sasa ni makavu, sasa ile Wizara imefanya utafiti wowote kujua ni kwa nini miradi inatumia mamilioni au mabilioni ya pesa lakini baada ya muda mchache inakuwa huduma ile haipatikani.

Tukiendelea na taratibu hizi Mhe. Spika, nafikiri tutakuwa tunayaendeleza tu miundombinu miundombinu, haja yetu ni kupatikana kwa maji safi na salama na sio kulaza mabomba, hivi sasa kila eneo mabomba yapo lakini maji hakuna, sasa kama ni wataalamu basi tumepeleka wataalamu wakajifunze, lakini uwezekano wa kupatikana maji ni mdogo, miundombinu ipo lakini sijui kwa nini maji hatupati. Nafikiri hiyo ndio ya kuona kwamba ni *challenge* na Wizara ifanye kazi ili itujuilishe au itupatie taarifa au wao wenyewe wawe na taarifa ya kutosha kujua kwamba kwa nini hivi sasa maji hayapo.
Mhe. Spika, miundombinu ya maji iliyotoka Kijichi kuelekea Saateni yalipita maeneo mengi yakiwemo Mtoni, Bububu na Kibweni, lakini leo ukienda baada ya Mtoni kuita mto imebadilishwa jina sio Mtoni kwa sababu kama si kwa nguvu za Mhe. Mazrui na juhudi zake basi wananchi wangelikuwa hivi sasa hawapati. Lakini la kushangaza unaweza ukaona ndani ya miezi sita imepita ukaja ukaona maji yanamwagika usiku hujui yametokea wapi, sasa inakuwaje Mhe. Waziri, kwamba leo miezi sita maji pale hayapo lakini siku moja ukayaona hayo yanakuja kwa nguvu kiasi mabomba yote yanapasuka, hii ni kuonesha labda utendaji wetu ni mbovu.

Mhe. Spika, kuna watu ambao wanafanya *sabotage* ya makusudi ili baadhi ya maeneo yakose maji, naomba hili tulione kwamba ni tatizo na uanze kulifuatilia.

Mhe. Spika, niende kwenye sekta ya umeme na nafikiri nitamalizia hapo. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba tunasaidia sana katika eneo la upatikanaji wa huduma ya umeme na nafikiri Waheshimiwa wengi wanapopata fedha zao huwa wanazipeleka katika kuwapatia wananchi katika majimbo huduma hii ya umeme. Ningewaomba Shirika kuna baadhi ya huduma wakachangia wao, hivi sasa inawezekana Mhe. Spika, kwa kupitia *CDF* akachangia nguzo pamoja na vifaa vyengine, lakini wanaku-*charge* mpaka *labour* wanakwambia ah! *labour* sijui, sijui mambo yao yanakuwaje. Nafikiri walio na jukumu la kusambaza umeme ni Shirika, lakini hawataki kuingia ubia na Waheshimiwa Wawakilishi.

Nafikiri ipo haja sasa ya kuona kwamba kwa vile Mwakilishi kachangia milioni kumi basi wao ile tano iliyobakia pengine waichangie wao ili tuendelee kuwasaidia wananchi wetu kupata huduma hii, tukifanya hivyo tutakwenda mbele. Lakini wakiweka mbele kwamba wao ni biashara wafaidike wao tu nafikiria wananchi watakosa huduma. Wajenge imani hiyo

kwamba na wao wanao wajibu wa kuchangia katika kuwapatia wananchi huduma hii, wanaofaidika zaidi ni wao kuliko sisi Waheshimiwa. Ahsante.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, na mimi sina budi awali ya yote kuweza kumshukuru Allah Subhanahu Wataalaa kunijaalia hali ya uzima na afya na kuweza kusimama katika kikao adhimu ili nitoe shukurani zangu za dhati kwako asubuhi hii ukaweza kunipatia na mimi fursa ya kutoa mawazo yangu katika hotuba hii ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Mhe.Ramadhan Abdalla Shaaban.

Mhe. Spika, mchango wangu utakwenda katika maeneo mbali mbali. Eneo la kwanza ni kifungu cha 97 ukurasa wa 21 hadi 24 pale na nitakwenda kimuhutasari sana. Kwanza kuna Idara ya Mipango Miji na Vijiji, hapa niipongeze sana Wizara kwa kupitia mipango yake hii ya Mipango Miji na Vijiji kwa hatua za mwanzo kabisa kuandaa sera. Mara tunapitisha sheria bila ya kuwa na sera, kwa hivyo hizi kwanza ni pongezi adhimu kuandaa sera kwanza ili kile kitachofuata kikawa tayari tumewekea njia ya kuongoza katika mipango yetu hiyo tuloiandaa. Lakini pia nipongeze zaidi kwa kutoa mashirikiano katika Taasisi ya Ardhi na Halmashauri zetu za Wilaya, kwani mbali ya Halmashauri zetu ujenzi huu na matumizi ya ardhi yanakwenda kwa kweli kiholela.

Mhe. Spika, mifano mbali mbali na tunajua kwamba Zanzibar ardhi yetu ni ndogo na baadhi ya maeneo mtu mmoja anachukua kubwa mno, ukiangalia Wazanzibari ni watu tunaozaa sana itafika hatua kizazi chetu kinachokuja wakose maeneo ya kuishi na watu wengi wanaojenga katika maeneo yetu wengi ni masikini, majengo yetu ni haya ya chini, hatujawa na mfumo ule wa kujenga *foundation* ya kudumu yenye uwezo wa kuchukuwa *flat* nyengine ziweze kwenda juu, kwa hiyo mtu mmoja anachukua eneo kubwa na ardhi yetu ni ndogo tutakuja kufika pahali kizazi kinachokuja ije iwe ni tatizo mwahala pa kuishi. Kwa hivyo kwanza naipongeza Wizara kwa suala hili na kuweza kuandaa mipango hii ili kuihifadhi uchache huu wa ardhi tulionao.

Pili Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 111 ukurasa wa 44, ukurasa huu unazungumzia elimu kwa watumiaji wa maji. Hili ni jambo la busara sana Wizara kwa kupitia Mamlaka ya Maji na kuendeleza kutoa taaluma kwa umma ya matumizi bora ya maji. Ni jambo la busara kwa kweli ni muhimu kupata taaluma maji Zanzibar yanatumika ovyo kiholela, hili ni tatizo.

Mhe. Spika, ukiangalia wakati wa Nabii Mussa Allayhi Salaam wale walikuwa na shida kubwa ya maji, kwa hivyo wakamfuata Mtume wao huyu Mussa awaombee kwa Mwenyezi Mungu ili wapate maji, kwa hiyo Nabii Mussa akapeleka maombi yale kwa Allah na akaambiwa na Mola wake

kwamba piga bakora yako kwenye jiwe, kupiga bakora yake jiwe ilivyokuwa kalijaalia likatoa chem chem kumi na mbili, ndani ya chem chem zile kumi na mbili na hawa watu anaowaongoza Nabii Mussa koo zao ni zile kumi na mbili, kwa hivyo kila ukoo pale wakajua maeneo yao ya maji, lakini Mungu aliwaambia vipi, musije mukayachawanya mukaleta uharibifu. Sasa kumbe Mungu hapendi kukuta watu wanaharibu maji ovyo ovyo.

Mhe. Spika, hapa Zanzibar suala hili lipo kwa hawa wenye kutoa elimu ya maji na hawa wenye kupewa elimu ya maji. Ukiangalia wananchi wetu wengi mifereji yao baadhi yao ni mibovu maji yanamwagika ovyo, lakini pia na hawa watu wa ZAWA sehemu yao ya mabomba makubwa maji yanamwagika ovyo. Kutokana na hali hii Mhe. Spika, wakati Mungu analikemea suala hili kwamba tusiharibu ama kama hatutojirekebisha tutachimba visima nyumba hadi nyumba lakini tutaendelea kuwa na tatizo la maji, tutaendelea kuwa na tatizo la maji kwa sababu uharibifu wa maji ni mkubwa mno.

Mhe. Spika, ukienda katika maeneo ya watu binafsi, tuangalie hapa eneo letu la Chukwani watu wengi wana visima vyao majumbani, lakini maji yanaharibiwa, bomba ndogo ndogo zinapasuka ovyo hakuna anayeshughulikia kuyaziba maji yale, lakini hata bomba kubwa ukianzia hapa Chuoni Karume pana bomba limepasuka maji yanapotea ovyo, ukija hapa Chukwani kwa Meya hapa utakuta kuna bomba linapasuka maji yanasambaa ovyo na maeneo mengine mbalimbali, sasa huu ni jumla ya uharibifu Mhe. Spika. Sasa ni bora tukaziba ufa kulikoni kuja kujenga ukuta, sasa tutalaumu kwamba maji hayatoshi na ni kweli hayatatosha kwamba kila tulichonacho hatuwezi kabisa kukidhibiti na tukakitoa katika mpangilio maalum.

Leo hapa ninashukuru Mhe. Spika, hawa wenzetu wa ZAWA hawa wameanza kuweka mita katika maeneo mbali mbali, lakini kwanza ningewashauri sana watu wa ZAWA mita hizi kwanza kabisa tukafungiwa sisi viongozi na taasisi zote za Serikali hatima yake sasa tukawaendea wananchi , lakini ZAWA huwaendea wale watu wadogo wadogo kwanza, kwa hivyo ili tutende haki tuweze kuyadhibiti maji basi lazima huu utaratibu tuanze kwa viongozi halafu tuwafuate wananchi ili na wao waone kwamba kama viongozi washaanza kufanya hivi basi na wananchi wetu ni rahisi mno kuweza kulikubali hili na kulifuata, na mimi naamini kwamba tutakapotumia mita hivi maji yatatumika vizuri na lile tone litakuwa na heshima yake, kwa sababu kila ukitumia maji mengi ndio utakapolipa pesa nyingi, kwa hiyo mtu akilipa mara ya kwanza mara ya pili basi mara ya tatu deni lile litakuwa ni kubwa ni lazima atakuwa na uangalifu zaidi wa kuyatumia maji.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika usambazaji wa maji vijijini. Nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri na Wizara yake kwamba

wamefanya jambo la busara sana katika kupeleka maji vijijini. Kwa kweli wananchi wetu wana tabu sana, maeneo yetu maji yako mbali sana wacha haya ya mabomba lakini hata yale ya visima vya ndoo, mtu anavuta maji hata akijaaza ile ndoo basi yuko taaban, yako chini sana inakuwa ni tabu kwa wananchi wetu na pengine kisima kimoja tu ndoo msongo uliopo, kwa kweli mtu kwa kweli mtu anakaa muda mrefu hajayapata hata hayo maji. Kwa hivyo kwa kuliona hili Wizara hii ya Ardhi, basi ni vyema harakati hizi zikaweza zikafuatwa na hii programu inayopangwa wananchi wetu wakaweza kuyamudu haya maji na kuweza kuondokana na shida hii kubwa ambayo wanaipata.

Mhe. Spika, hapa kidogo ninataka nizungumzie suala zima la Shirika la Umeme, *paragraph* ya 140 hadi 141. Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati imechukua jitihada kubwa katika suala zima la kukuza ubora wa huduma ya umeme kwenye maeneo yetu. Hapa hatuna budi kutoa shukurani zetu za dhati kabisa. Lakini kutokana na hali yao hiyo, kuna vijiji vyetu vingi Unguja na Pemba huduma hii adhimu bado kabisa haijafikiriwa.

Kwa hiyo naomba kwamba katika vijiji vingine hasa kushuhudia hii anga hili la taa basi hawalioni, wako mbali na mambo haya ya umeme. Kwa hiyo naomba sana vijiji vyetu hivi viweze kufikiwa na nguvu hii.
Mhe. Spika, katika Jimbo langu kuna vijiji mbali mbali ambavyo bado havijapata huduma hii ya umeme na vijiji vingine tumeshafuatilia sana katika Shirika la Umeme lakini kila siku tunaambiwa bado hatujapata wafadhili na mambo mengine, vijiji vyenyewe kama Mgeni Nje, Patini, Gombe, Mambosasa, Rahaleo, Mnazi Mmoja, Uwondwe na maeneo mengine hayajabatika kupata huduma hii, na hao ni walipa kodi kama vijiji vingine ambavyo tayari hii huduma washaipata. Kwa hiyo namuomba sana Mhe. Waziri, ajitahidi sana suala hili ili vijiji hivi viweze kufanikisha na wao ili waweze kupata umeme huu kama wanavyopata vijiji vingine.

Lakini pia la mwisho kwa kumalizia Mhe. Spika, naomba tu ufafanuzi katika kiambatanisho L ukurasa wa 98 na 99. Hapa kuna vijiji vilivyopatiwa huduma za umeme kupitia mradi wa usambazaji wa umeme vijijini kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Mhe.Spika, kuna vijiji hapa hasa kijiji kimoja cha Kijichi, hivi vijiji vyengine vyote vimefanikiwa ni lipi lililosababisha hawa wakakosa huduma hii naomba nipate taarifa. Lakini kuna hizi gharama naomba nipate maelezo gharama hizi ni Shirika lenyewe waliogharamia au ni vijiji wenyewe wamegharamia fedha hizi, hapa naomba Waziri atakapokuja anipe naelezo ya kina ili niweze kutoa na kupeleka fikra hizi kwa hivyo vijiji ambavyo vimo katika Jimbo langu na majimbo mengine. Ahsante, naunga mkono hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sijakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa fursa hii kuchangia Wizara ambayo muhimu au uti wa mgongo wa nchi hii ikiwemo maji, nyumba, makaazi bila ya vitu hivi huwezi kuishi.

Mhe. Spika, nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwa jitihada anazochukua katika Wizara hii. Waziri ambaye ametumikia Serikali hii karibu miaka 35. Baada ya hapo ninataka nimshukuru Mhe. Naibu Waziri, ndugu yangu, rafikiri yangu Mhe. Haji Mwadini anayeongoza Wizara hii na baada ya hapo nimpongeze Katibu Mkuu aliyekamata karibu mara mbili Wizara, na hii inaonekana kutokana na utendaji wake na umakini wake kupewa Wizara hii na uwezo wake.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze na ukurasa wa 32 Mamlaka ya Hifadhi ya Maji Mkongwe. Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa mamlaka hii imekuwa ikifanya kazi sijui tuseme kwa ubaguzi au vipi, tumelia sana na njia ya Forodhani kufungwa.

Njia ile Mhe. Spika, inasumbua sana na hakuna sababu mpaka leo serikali njia ile kushikilia kuifunga, kama kufunga wafunge eneo la Bandarini pale, pale ndipo penye msongamano wote. Leo cha kushangaza pana magari makubwa makubwa ya mawe yanapita, lakini wananchi wa nchi hii hawaitumii njia ile anakuja kutumia mgeni ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Spika. Mhe. Waziri atapokuja hapa nataka maelezo kuhusu njia ile na hii ni mara ya pili kuchangia.

Juzi Mhe. Salmin Awadh alipiga kelele kwa Mhe Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nakumbuka Dr. Mwinyihaji alikuwa msikivu kwa njia ile, mimi nakumbuka niliuliza swali na siku ya pili akatoa amri akaifungua ile njia. Sasa nataka kujua Mkurugenzi na Waziri nani mkubwa katika nchi hii? Kama mkubwa Waziri keshatoa amri leo anakuja Mkurugenzi anapinga ni kitu cha kusikitisha sana. Njia ile inasumbua watu na kuna hatari ya kuja kutokea ajali penye tobo Nyumba ya Kulelea Watoto pale.

Baraza hili niliuliza swali mimi nikaambiwa kwamba mahoteli sasa hivi Mji Mkongwe yamepigwa marufuku na sasa mahoteli yanazidi kuendelea sijui marufuku hiyo iko wapi?

Eneo la Bandarini mle ndani mote mmevunjwa umebakia ule ukuta tu, mimi ningeomba na ule ukuta uliobakia nao ukavunjwa, kwa sababu ni sawa sawa na kufunga mlango wa nyumba mbele na wa nyuma ukauacha wazi. Pale pamekuwa na msongamano mkubwa kweli kweli wa magari, ule ukuta

uliobakia kama unaonesha sura ya Mji Mkongwe ilikuwa hakuna sababu ya kuvunja, ukuta ule ningemuomba sana Mhe. Waziri palipobaki pale akamaliza.

Mhe. Spika, mwenzangu Mhe. Saleh Nassor Juma jana alichangia sana hapa kuhusu Mzee wetu aliyetumikia taifa hili aliwahi kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa, vile vile alikuwa Halmashauri Kuu ya Taifa, alikuwa Waziri katika mwaka 1995 – 2000. Vile vile alikuwa Mhe. Naibu Spika, karibu miaka 10 kutoka 2000 – 2010 kama si Mhe. Nassor Salim Ali kumuangusha nadhani mpaka leo angekuwa Naibu Spika. Huyu mtu kwa kweli hali yake inasikitisha hivi sasa, kile kiwanja mngemsaidia kama suala la kujenga kituo cha petroli limekataliwa, cha kusikitisha hivi sasa Mhe. Spika, pana maduka yanaendelea kujengwa hivi sasa kama si ubaguzi ni kitu gani. Pana maduka huku Umoja wa Vijana wanajenga na huku pembeni kuna maduka mengine yamejengwa nayafahamu, kama ni kisingizio *transformer* mita kumi haifiki Mhe. Spika, twende tukapime lile eneo, mtu kama huyu keshatumikia nchi hii si asaidiwe.

Mhe. Saleh Nassor alisema isije ikafika wakati akauza moto, moto mikate jana kasema hapa Mhe. Saleh, kiongozi kama yule nchi hii inabidi kuondoka humu tena hawezi kuenziwa? Mhe. Waziri naamini huyu alikuwa Waziri mwenzio kwa hili na ninavyokufahamu mimi nafikiri utalipatia ufumbuzi, kama suala la kituo haiwezekani wafanye biashara nyengine kama wale wengine walioruhusiwa. Katiba ya Zanzibar ukurasa wa 7 hakuna ubaguzi, Mheshimiwa naomba kunukuu.

Kifungu 11(1) kinasema kwamba:

> "Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa.
>
> (2)Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.
>
> 12(1) Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.
>
> (2) Hakuna sheria itakayokuwa na kifungu chochote ambacho ni cha ubaguzi wa moja kwa moja au kwa taathira yake".

Mhe. Waziri hapa nitahitaji maelezo ya kina yule mzee wetu sasa hivi hiyo nyumba anayokaa *Wallahi* itakusikitisha, sasa hivi anaambiwa aondoke pale, mtu keshatumikia miaka mingapi nchi hii. Namuomba sana Mhe. Waziri mimi najua ni msikivu kwa hili nafikiri utamsaidia ni muasisi wa nchi hii. Maana kama haiwezekani kujenga kituo pale pana maduka hivi sasa

yanajengwa Mhe. Waziri twende tukakague haifiki mita tano ilipo *transformer* ya umeme na huku maduka mengine yamejengwa juzi tu.

Mhe. Spika, hata Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema ukurasa wa 2013, "Kuendelea kupiga vita, kudhibiti na kutoruhusu vitendo vya ubaguzi wa aina yoyote, ili kujitokeza katika sehemu za utoaji wa huduma au fursa mbali mbali za kiuchumi au kijamii miongoni mwa wananchi". Ilani yetu ya uchaguzi hii inakataza mambo hayo. Mhe. Spika, nitahitaji maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri na nimuombe sana yule mzee amsaidie na atalipwa na Mwenyezi Mungu.

Baada ya hapo nije katika Mipango Miji. Mhe. Spika, idara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi, kwa nchi zinazoendelea na maendeleo kuonekana hupiga sura ya mji. Mimi hapa nitahitaji maelezo ya Mhe. Waziri, huu mji mpya wa Zanzibar ni Chukwani, Kinyasini, Fumba, maana sijaona mji mpya mimi, kama ni mji mkuu kweli Tunguu kuna huduma mbona hazipatikani magari yanasimama ovyo tu kule. Mhe. Spika, haiwezekani mtu atoke Chukwani akafuate masuala ya benki mjini sijui *master plan* ya mji huu itakuwaje masoko ni kitu muhimu kupangwa. Leo daladala zinavyosimama njiani huwezi kuamini, hii ni kutokuwa na mipango miji.

Jengine nimuombe sana Ndugu Dr. Mohamed wa Mipango Miji, anachotaka kufanya kuondosha Bandari ile kule Forodha Mchanga ahakikishe serikali itakosa pesa nyingi sana. Hili nafikiri atakuwa halijui ndio namchangia kumpa mawazo mapema. Zanzibar hivi sasa biashara yake inayotegemea ni magari tu, kutokana na ushuru Tanzania Bara kuwa ni mkubwa kuliko Zanzibar, hili Waziri wa Fedha alizungumza atalisimamia na pale kama meli inakaa ni dakika 15 au 20 tu hakuna sababu ya kufunga, wale ni wawekezaji wazalendo hata Mhe. Rais juzi katika kufungua Bandari alisema *priority* wazalendo. Wewe nambie gari shehena zinazopakiwa pale ushuru gari moja shilingi milioni mbili au tatu leo unakuja kuondosha wanakwenda wapi.

Dr, Mohamed kwa heshima na taadhima kabisa suala hili nakuomba uliangalie, hili nafikiri ulikuwa hujui kwa sababu pana kodi serikali inapata pale. Ndugu zetu wa Bara ushuru wao wa magari umekuwa mkubwa, wenzetu wanapotoka Bara wanakuja hapa kutoa gari kupata nafuu leo unataka kuondosha watu wale Forodha Mchanga uwapeleke wapi na mji wetu ndio huu.

Sasa nije kwenye Vianzio vya Maji ukurasa wa 37. Hapa nafikiri Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Waziri suala hili wakati wowote tuunge bomba mpaka Bagamoyo tupate maji. Na kwa kuyatumia maji ya bahari kutokana na gharama zake ni kubwa. Bado tumekuwa na kazi ngumu sana kwa Mamlaka

ya Maji, mimi wala siwezi kulaumu katika watu wenye nidhamu kwa upande wangu mimi niwashukuru sana watendaji wa Mamlaka ya Maji akiwemo Mkurugenzi Mkuu Bwana Mustafa, Mkurugenzi Ufundi Bwana Ilyas, Mkurugenzi Mshika Fedha bwana Ali Tamim. Kwa kweli wamenipa mashirikiano makubwa tokea kuingia katika Baraza hili, tunashukuru sana na waendelee hivyo na Wakurugenzi wengine niombe wawe na mfano huo ni watu wanaoonesha nidhamu.

Lakini Mhe. Spika, hawa kitaalamu siku zote wakati vitendea kazi hawana watafanya kazi vipi na bajeti yao ni ndogo. Hapa nitahitaji maelezo sana kwa Mhe. Waziri kuhusu bajeti ya Mamlaka ya Maji. Tuangalie kwenye majumba ya Michenzani yale tangu yalipojengwa hayajabadilishwa rangi mpaka leo na yale yanalipiwa, tokea yalipojengwa na Muasisi wa nchi hii zile nyumba hata kubadilishwa tunashindwa, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi.

Mhe. Spika, pana jumba lililobaki lile Mhe. Saleh Nassor alizungumza ni aibu mpaka mwanawe ndio kaja kumaliza, hebu tuenzi jitihada za wazee wetu walizozifanya. Hapo mwanzo yalikuwa yakitoka maji mpaka juu sasa hivi maji hayapatikani Michenzani, yangewekwa angalau mapipa mle chini katika kipindi hiki watu wakatoka juu wakaja wakachota maji.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nitakuwa mgumu kama sijapata maelezo yanayohusu kiwanja kilichopo Umoja wa Vijana kinachomilikiwa na muasisi wa nchi hii ambaye sasa hali yake hoi bin taabani.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kuweza kuichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, natanguliza kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya leo na mimi kuichangia hotuba hii. Kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri na nampongeza kwa dhati kabisa kwa jinsi anavyoitumikia na anavyojitolea katika kuhangaika huku na kule na hatimaye kutuletea maendeleo Wananchi wa Zanzibar. Katibu Mkuu wake, Naibu Katibu Mkuu pamoja na wasaidizi wake wote, Wakurugenzi pamoja na watendaji wengine. Ni imani yangu kwamba ufanisi wake wa kazi unatokana na mashirikiano mazuri aliyoyajenga katika wizara yake.

Lakini kwa dhati kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jinsi alivyokuwa karibu sana na wizara zetu na hasa suala hili la huduma ya jamii likiwemo

suala la maji na umeme. Mchango wake mkubwa katika wizara hii umesaidia sana kuleta ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, nimesimama hapa kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwanza kuunga mkono hotuba ya Waziri kwa asilimia mia moja. Na wananchi wa Jimbo la Makunduchi wamenipa salamu zao kwa Waziri ambazo nitazisema baadae kidogo. Lakini kwanza naomba nianze na suala zima hili hili la Nyumba za Maendeleo.

Jimbo la Makunduchi tumebahatika katika maeneo ya Zanzibar kupata nyumba zile za Maendeleo. Mhe. Spika, nyumba hizi Waheshimiwa wengi wamezizungumzia kwamba nyumba hizi zinaonekana kama zilivyo hali yake sio nzuri. Mimi nataka nimpe ushauri Waziri na sisi kama ni viongozi wa majimbo tunayo nafasi vile vile kwa njia moja au nyengine kuchangia katika suala zima la nyumba hizi na baadhi yetu tunakaa humo humo.

Mhe. Waziri nyumba hizi ziko katika hali mbaya sana, mimi ningemshauri kama kuna uwezekano mkubwa wa kuzifanyia ukarabati kidogo basi sisi Wawakilishi na Wabunge wa majimbo ambao tumebahatika kuwa na nyumba hizi tushirikishwe ili tusaidiane kutafuta mbinu na njia mbali mbali, ikiwezekana hata kuunda kamati ndani ya maeneo yetu ili kuhakikisha kwamba nyumba zile tunazirejesha katika heshima ambayo ilikuwanazo. Kwa masikitiko makubwa hali ya nyumba hizi Mhe. Spika, zinaendelea kuharibika na wananchi wanazitumia bado. Mimi nasema hivi kwa sababu ya nia kuwa sisi kama Wawakilishi tuna wajibu na sisi kusaidia katika suala zima la kuziimarisha nyumba hizi.

Suala la pili Mhe. Spika, ni suala la maji. Hili naomba nikushukuru sana, katika juhudi zako za kutafuta maendeleo ya nchi hii umekwenda Ras-el-Khaima na *Alhamdulillah* umetuletea visima 50 msaada huo ambao tumeupata. Tunakushukuru sana Mhe. Waziri.

Kwa bahati nzuri sana kwa imani yako kwa wananchi wa Jimbo la Makunduchi umewatengea sehemu ya kuchimba visima hivyo. Mheshimiwa nakushukuru sana, ninachokuomba tu mimi kama kukupa ushauri, wakati wataalamu wako watapokuwa tayari kwenda kuchimba visima katika maeneo hayo kwa sababu na sisi Wawakilishi na Wabunge tumechimba visima zaidi ya 12 katika maeneo mbali mbali, basi naomba tushirikishwe katika uchimbaji wa visima vile ili tujue hasa wapi wanataka kuvichimba, kwa sababu kuna maeneo ambayo sisi tunayajua yana matatizo zaidi ya maji kuliko maeneo mengine.

Mhe. Spika, maeneo kama ya Mtende kuna matatizo Mhe. Waziri, Makunduchi kwa ujumla, Kizimkazi na maeneo mengine katika jimbo hilo kuna matatizo ya siku nyingi ya maji. Lakini wananchi wa Jimbo la Makunduchi kama alivyokuwa Mwakilishi wao ni watu wenye subra sana, sasa tujitahidi Mhe. Waziri.

Lakini pia Mhe. Spika, tuna tangi letu la maji, tangi hili Mhe. Rais alipokwenda kule aliahidiwa kwamba lingefanyiwa matengenezo na sisi tukajipima, tukajipiga kidogo tukasema tutasaidia kuchimba visima kwanza kwa wakati huo tukisubiri matengenezo haya. Wananchi wa Jimbo la Makunduchi hivi sasa hawafurahii yale mambo ambayo wanayaona kwenye mitandao. Baadhi ya wananchi wetu ambao ni wazaliwa wa huko huko lakini kwa sababu tu wanataka kuidhalilisha serikali na pengine wanafikiri wanamdhalilisha Mwakilishi wao, basi huweka lile tangi la maji Makunduchi wakasema tangi lipo lakini halina maji. Sasa wao vita vyao viko kwa Mwakilishi pengine, lakini suala la kupeleka maji si jukumu la Mwakilishi peke yake ni sote ambao tunahusika katika serikali hii.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri nilipata taarifa kwamba bajeti iliyopita mlitenga pesa fulani karibu shilingi milioni mia moja nashukuru sana, sasa mwaka umemalizika bahati haikuwezekana. Naomba sana mwaka huu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi Mheshimiwa, nakuomba kwa sababu suala hili la maji ni muhimu na wakati huu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani wanapata shida, najua hatuwezi kulitengeneza tangi lile kwa leo na kesho kwa sababu gharama zake ni kubwa. Lakini nimuombe sana tangi lile sasa imefika wakati tusiwape nafasi hao wachache wapinga maendeleo wanaojinata huko kwamba wao ndio wanataka maendeleo zaidi kuliko wenzao, wakaanza kuweka matangi yale kwenye mitandao, na si kwa nia yoyote ila ni kuidhalilisha serikali.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ana wafanyakazi wazuri sana nina hakika, wasikivu, na nina hakika kama hili litasimamiwa basi wananchi wa Jimbo la Makunduchi watafaidika sana. Mhe. Waziri anafanya kazi kubwa sana, inawezekana hawezi kuiona kama Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliyeondoka Koffi Annan alisema kwamba, unapofanya jambo la kimaendeleo huwezi kuliona wewe moja kwa moja kama vile unavyoweza kujiona kwenye kioo. Kwenye kioo unajiona kama ulivyo, lakini suala la maendeleo wewe utakuwa unafanya lakini wanaoona ni wengine. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tujitahidi sana.

Suala jengine Mhe. Spika, ni suala la umeme, kwanza hapa naomba nichukue nafasi hii Mhe. Spika, nimpongeze sana Mkurugenzi wetu wa *ZECO*, kijana

huyu anajitahidi anafanya kazi nzuri sana kama alivyo Mkurugenzi wa maji, wote hao wanafanya kazi vizuri sana chini ya uongozi wa Waziri.

Mhe. Spika, naomba sana, natishika kidogo na mengine nilimnong'oneza Mhe. Waziri nikamwambia na mengine nitamwambia baadae mimi na yeye tutapokaa zaidi, lakini namuomba sana Mkurugenzi huyu wasaidizi wake walio chini yake tujitahidi kuwaangalia vizuri. Kwa sababu *image* ya idara hii wanaweza wakaleta athari, nadhani nikisema hivyo inatosha kwa sababu sitaki kwenda kwenye *detail* zaidi. Lakini juhudi ambazo anazifanya Mkurugenzi binafsi ndizo ambazo zinafanya *ZECO* ionekane kwamba inafanya kazi vizuri. Wako wasaidizi wake wazuri, lakini bado kuna wengine wanaleta matatizo pale.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kuna manung'uniko mengi katika Jimbo la Makunduchi wakati mwengine kukata umeme tu hata kutoa mita vile vile jambo ambalo ni zito sana hilo. Hivyo naomba sana hili aje anipe nafasi baadae *Inshaallah* atapopata nafasi baada ya kufanya majumuisho yake ambayo tutayaunga mkono kwa asilimia mia moja basi tufike mahali hili aliangalie vizuri.

Mhe. Waziri nampongeza sana juhudi ambazo amezichukua kwenye maeneo ya ardhi na naomba juhudi yake iendelee. Mheshimiwa anafanya kazi nzuri na Mwenyezi Mungu atamsaidia tukijaaliwa na sisi tuko pamoja na yeye.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka nilete hizo salamu za wananchi wa Jimbo la Makunduchi na wamenituma. Mwaka juzi walinituma sikuyasema kwa sababu nilisema kwa njia ya maandishi, mwaka jana walinituma vile vile nikachangia kwa maandishi hasa suala la maji. Sasa mwaka huu wamenambia hebu tukusikie sauti yako na wewe usije ukaonekana bubu, ingawa tuna asili kidogo wazee wetu wengine mabubu, lakini ndio mambo na mimi sio bubu *Alhamdulillahi*.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nakushukuru sana Mwenyezi Mungu ajaalie bajeti hii ipite ni wizara nzito na Waziri anahitajia tumsaidie, jukumu hili la wizara si lake peke yake ni letu sote. Basi Mhe. Spika, baada ya hayo machache sana niliyozungumza naomba sana niunge mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi na kuwaomba wananchi wote na Wawakilishi tuunge mkono hoja hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika nakushukuru, Waheshimiwa Wajumbe pia nawashukuru kwa mashirikiano ambayo mmeyatoa katika kuchangia hotuba ya wizara hii. Wachangiaji walikuwa wengi tumejaribu kujitahidi na tumefanikiwa kufikia

michango ya Wajumbe kama 20 hivi, lakini Mhe. Waziri aliniambia mapema kwamba ana bahasha nzima ya michango kwa maandishi, ilibidi iwe hivyo kwa sababu muda wenyewe nao umekuwa finyu.

Kwa hivyo, mniwiye radhi Waheshimiwa Wajumbe kwamba mchangio wa Mhe. Waziri wa Kazi kwa leo unahitimisha michango imebakia kuwasikiliza wenyewe Mungu akipenda siku ya Jumatatu. Kuna baadhi ya Wajumbe walinambia kwamba kwa nini hatuwaombi Waheshimiwa Wajumbe tuje baada ya Ijumaa, lakini nikaogopa nisije nikakataliwa. Sasa kuna makofi kidogo sana yamejitokeza hapa ingekuwa yako mengi basi ningemwambia Mhe. Waziri atoe hoja, lakini kwa kuwa si mengi naogopa kushawishi itolewe hoja hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe basi baada ya hayo sasa niakhirishe kikao hiki hadi siku ya Jumatano tarehe 15/07/2013 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 5:50 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 15/07/2013 saa 3:00 asubuhi)